SportPesa
TZS. 710,494,580
NI YA KWAKO WIKI HII, BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Mkuu** TAZARA akana kupokea washtakiwa katika kesi ya Mbowe

UKURASA 3



**Pochettino azungumzia tetesi kutua Man United**

UKURASA 23

Nipashe
Alhamisi Novemba 25, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580775
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Wanaopewa ujauzito sasa kurudi shuleni

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**907,802 WACHAGULIWA KIDATO CHA KWANZA**
WANAFUNZI 907,802 waliofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi...

UKURASA WA 8
**SHAHIDI AELEZA SABABU ZA KUTOA MILIONI 90/-**
SHAHIDI wa 10 wa Jamhuri Francis Mroso (44), katika kesi ya uhujumu...



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (katikati), akishuhudia utiaji saini mkataba wa ushirikiano wa uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, baina ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Dubai National Air Travel Agency, Ikulu jijini Zanzibar jana. Wanaotiliana saini ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Amour Hamil Bakari (kulia) na Mkurugenzi wa Biashara wa Kampuni ya EGIS, Cristian Laugier. **PICHA: IKULU**

## Jambazi auawa baada ya kupora kituo cha mafuta

UKURASA 3



## Makalla asema maji bado shida, ataka maombi mvua inyeshe

UKURASA 2

MICHEZO **AUCHO AITULIZA YANGA SC** UK.24
**MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdallah, wakizindua matokeo ya utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi 2020/2021, jijini Zanzibar, jana. Kushoto ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira, Vijana, Kazi na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama. **PICHA: OWM**

# Wanaopata ujauzito kurejeshwa shuleni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema itaendelea kuondoa vikwazo katika upatikanaji wa fursa za elimu ikiwamo kuruhusu wasichana waliopata ujauzito wakiwa shule za msingi na sekondari kuendelea na masomo katika mfumo rasmi.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alibainisha hayo jana alipokuwa akitoa taarifa ya mafanikio ya sekta ya elimu kwa waandishi wa habari katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika.

Alisema wanafunzi waliokatiza masomo yao kwa sababu mbalimbali watapewa fursa ya kurejea shuleni.

"Fursa hizo zitajumuisha wasichana ambao wanapata ujauzito wakiwa katika shule za msingi au sekondari, wanafunzi hao wataruhusiwa kuendelea na masomo katika mfumo rasmi baada ya kujifungua," alisema Prof. Ndalichako.

Alisema wanafunzi wengine ni wale ambao wanaobainika kufanya udanganyifu katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi ambao matokeo yao hufutwa na wale wanaoshindwa kufaulu mtihani au wanaopata matatizo yoyote wakati wa mitihani pia watapewa fursa ya kurudia mtihani mwaka unaofuata.

Kutokana na wanaoshindwa kufanya mitihani, alisema Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania (NECTA) litatoa utaratibu wa kurudia mitihani. Pia alisema wanafunzi ambao watafaulu mitihani ya marudio watapata fursa ya kuchaguliwa kuendelea na masomo ya sekondari katika shule za serikali.

Kutokana na hali hiyo, alisema serikali imeona umuhimu wa kuwapa nafasi ya pili wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi kama inavyofanyika kwa wanafunzi wa sekondari.

Pia alisema serikali itahakikisha kuwa hatua kali za kinidhamu zinachukuliwa dhidi ya watumishi wote watakaobainika kuhusika na udanganyifu katika mitihani yote ya Taifa.

"Wasione kwa kuwa tumetoa fursa hii basi ndiyo wajihusishe na vitendo vya udanganyifu wizara yangu itaendelea kuwachukulia hatua kali watumishi wote watakaobainika na udanganyifu wa mitihani mbalimbali," alisisitiza Prof. Ndalichako.

Kadhalika, alisema kuwa serikali itaendelea kutoa elimu bila malipo ili kuhakikisha kuwa watoto wote wakitanzania wanapata elimu bila vikwazo. "Aidha, serikali itaendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu katika mwaka wa fedha 2021/22 bajeti iliyoongezeka kutoka Sh. bilioni 464 hadi 570," alisema.

Sambamba na hayo, alisema serikali itaendelea kuboresha elimu, sayansi na teknolojia kwa ajili ya kuleta maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.

Alisema serikali itahakikisha kuwa inaboresha mitaala ya elimu katika ngazi zote na kuweka msisitizo zaidi katika masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Sayansi, Ujasiriamali, Stadi za Kazi na masuala mtambuka. Ndalichako pia fani za kimkakati kama vile uhandisi, kilimo, udaktari zitaendelea kupewa kipaumbele na serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya shule ili kuendelea kutoa fursa zaidi kwa watoto wa kike na wa kiume.

"Kazi hii inafanyika kwa kasi zaidi ambapo sambamba na ujenzi wa madarasa 15,000 unaoendelea nchini serikali inatarajia kujenga shule 1,000 za sekondari za kutwa na shule za sekondari 26 za wasichana katika kipindi cha miaka mitano ijayo," alisisitiza Prof. Ndalichako.

# Makalla adai maji bado shida, ataka maombi mvua inyeshe

**Na Frank Monyo**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amesema hali ya upatikanaji wa maji si ya kuridhisha, hivyo amewataka wakazi wa huo na wa Pwani wanaotumia maji kuwaa waangalifu katika utumiaji wa huduma hiyo.

Makalla alisema hayo jana baada ya kutembelea mitambo ya kuzalisha maji ya Ruvu Chini na Ruvu Juu na kujionea hali halisi, hivyo kuwataka wananchi kuyatunza maji wanayoyapata.

Akiwa na kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa kwenye ziara hiyo, alisema wananchi wanapaswa kuendelea kutunza vyanzo vya maji na maji yanayopatikana kwa sasa na kuyahifadhi kwa kuwa hali bado haijarejea.

Mkuu huyo wa mkoa alisema serikali imeshafanya jitihada zake za kukabiliana na mgawo wa maji, hivyo kilichobaki ni viongozi wa dini na wananchi kufanya maombi mvua zinyeshe ili kina cha maji kiongezeke kwenye vyanzo vya maji.

Katika ziara hiyo, Makalla na kamati yake walijionea hali halisi juu ya kupungua kwa kina cha maji katika mto huo kulikosababishwa mabadiliko ya tabia nchi pamoja na shughuli za kibinadamu.

Aliwata watu kutobweteka kutokana na kauli iliyotolewa mwishoni mwa wiki kuwa kuna nuru ya kupungua kwa mgawo wa maji baada ya kudaiwa kuwa kina cha maji kimeongezeka baada ya mkulima aliyekamatwa akivuta lita milioni moja kukamatwa.

"Watu walimwelewa vibaya Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA (Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam), (Mhandisi Cyprian Luhemeja) aliposema baada ya operesheni kumetokea ongezeko kidogo la maji. Watu wakaandika kwa sasa upatikanaji wa maji ni asilimia 100. Leo (jana) nimesema kuna upungufu na nimekuja, nimeona maana kuona ni kuamini," alisema.

Alisema mahitaji ya maji kwa wananchi wa Dar es Salaam ni zaidi ya lita milioni 540 kwa siku lakini uzalishaji hasa unakuwa lita milioni 520 na vyanzo vikubwa vya maji hayo ni Ruvu Juu na Ruvu Chini.

"Ruvu Juu Kwa siku wakifanya kazi katika 'full capacity' (ukamilifu) kwa siku wanazalisha lita milioni 196 na Ruvu Chini wakifanya 'full capacity', production (uzalishaji) wake ni lita milioni 270.

"Mtambo wa Ruvu Juu hali ipo sawa kwa asilimia 90 kwa hiyo wanacheza kwa uzalishaji wa lita milioni 196 na milioni 180. Hapa tulipokuja (Ruvu Chini) panatakiwa pazalishwe lita milioni 270 lakini hali tuliyoiona sasa si nzuri. Maji yamepungua sana. Tunampongoza Mheshimiwa Rais Samia (Suluhu Hassan) kwa maelekezo yake pamoja na Waziri Mkuu kwa wakuu wa mikoa, chanzo cha kupungua maji ni nini," alisema.

Aliongeza kuwa wakati tamko linatoka uzalishaji wa maji Ruvu Chini ulikuwa lita milioni 68 kutoka kita milioni 270.

# Mbinu tano kukabili kupanda vifaa ujenzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetaja hatua tano za kukabiliana na kupanda kwa bidhaa za ujenzi huku ikiagiza Tume ya Ushindani (FCC) kufanya uchunguzi na kuchukua hatua kisheria kwa waliopandisha bei ya saruji isivyo halali.

Aidha, imezuia usafirishaji wa shaba chakavu nje ya nchi ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa za chuma nchini.

Hatua nyingine ni kuiagiza FCC kuendelea kufuatilia mwenendo wa upandaji bei na kuwachukulia hatua stahiki wafanyabiashara wanaokiuka sheria ya ushindani, kupiga marufuku uuzaji nje ya nchi shaba chakavu.

Nyingine ni kurekebisha sheria na kanuni ili kuruhusu kuingizwa kwa urahisi zaidi malighafi zinazohitajika katika uzalishaji wa bidhaa za vyuma ikiwamo kuruhusu kuingizwa kwa vyuma chakavu kutoka nje kwa utaratibu utakaohakikisha inapatikana bila kuathiri mazingira ya nchi.

Pia katika mpango wa muda mrefu, serikali itatekeleza miradi kielelezo itakayowezesha kuzalisha chuma kingi nchini kwa ajili ya viwanda vya ndani na kuuza nje ya nchi.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, alibainisha hayo jana jijini hapa wakati akitoa tathmini ya mwenendo wa uzalishaji, usambazaji na bei za vifaa vya ujenzi kwa kipindi cha Septemba hadi Novemba, mwaka huu.

Alisema wizara hiyo imekuwa ikifanya tathmini ya mara kwa mara ya mwenendo wa uzalishaji, usambazaji na bei za bidhaa muhimu nchini zikiwamo vyakula, sukari, mafuta ya kula na vifaa vya ujenzi hususani saruji, mabati na nondo.

Pia alisema tathmini ilifanyika katika mikoa tisa inayotumia zaidi bidhaa hizo ambayo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza, Pwani, Shinyanga na Ruvuma.

Akizungumzia kuhusu saruji alisema nchi ina viwanda tisa vinavyozalisha bidhaa hiyo vyenye uwezo wa kuzalisha tani 9,080,000 kwa mwaka. Alisema matokeo ya tathmini yanaonyesha kuwa katika mikoa hiyo bei za saruji zimepanda kwa wastani wa Sh. 1,000.

Alitolea mfano mkoa wa Mwanza ambao bei imeongezeka kutoka Sh. 19,000 kwa mfuko wa kilo 50 kwa Septemba hadi kufikia Sh. 20,000 mwezi Novemba.

Pia kwa mkoa wa Dar es Salaam, alisema bei imepanda kutoka Sh. 14,000 kwa mwezi Septemba hadi Sh. 15,000 Novemba mwaka huu huku Ruvuma bei ikishuka kwa asilimia 15 kutoka Sh. 17,000 hadi 14,500 kwa kipindi hicho.

"Kupanda kwa bei za saruji katika kipindi cha tathmini kulisababishwa na mfumo wa usambazaji wa bidhaa hiyo na hakutokani na kupanda kwa gharama za uzalishaji viwandani. Kwa sababu hiyo ongezeko la bei linachukuliwa kuwa halikuwa halali," alisema Prof. Mkumbo.

HABARI KITAIFA

# Shahidi akana kuwapokea washtakiwa kesi ya Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

ALIYEKUWA Kaimu Mkuu wa Kituo cha Polisi TAZARA, Inspekta Lugawa Maulid, ametoa ushahidi wa kitabu cha kumbukumbu za mahabusu (DR) waliokuwa wakiwashikilia huku ikibainisha kuwa majina ya washtakiwa wa pili na wa tatu katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, na wenzake watatu hayamo.

Shahidi huyo wa Jamhuri pia amekana kupewa jukumu la kuwahifadhi mshtakiwa wa pili, Adamu Kasekwa na wa tatu, Mohammed Ling'wenya, ambao wanadai hawakuwahi kufikishwa Kituo cha Kikuu cha Polisi Dar es Salaam bali walifikishwa Kituo cha TAZARA Agosti 7, 2020.

Inspekta Maulid ambaye ni shahidi wa nne kwenye kesi ndogo, alidai hayo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, mbele ya Jaji Joachim Tiganga, alipokuwa akiongozwa kutoa ushahidi na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando.

Maulid alidai yuko Kituo cha TAZARA kwa miaka 17 na Agosti 3, 2020 alipewa jukumu la kukaimu nafasi ya mkuu wa kituo baada ya aliyekuwapo kwenda likizo ya siku 28. Alidai kuwa alianza jukumu hilo kuanzia Agosti 3 mpaka Septemba 6, 2020 Mkuu wa Kituo, Richard Ogutu, aliporejea na kwamba Juni 3, mwaka huu, alipata jukumu la kukaimu tena baada ya Ogutu kuhamishiwa Zanzibar.

Inspekta Maulid alidai Agosti 7 mpaka 9, 2020 alikuwa kazini Kituo cha Polisi TAZARA akitekeleza majukumu yake.

"Agosti 7, 2020 nilifanya ukaguzi katika mahabusu yetu ya TAZARA haikuwa na watuhumiwa. Agosti 8, 2020 nilifanya ukaguzi wa kawaida, palikuwa na mahabusu mmoja, Godfrey Kilimba, aliyekuwa anatuhumiwa kujifanya mtumishi wa serikali.

"Agosti 9, 2020 kulikuwa na watuhumiwa wawili wanafunzi wa kiume, John Gerald na Lucas Jovin ambao walikuwa wanatuhumiwa kuhatarisha miundombinu ya reli. Tuliwakamata wanafungua nati za reli, walitoka Agosti 10, 2020," alidai.

Alidai watuhumiwa hao walikuwapo mahabusu katika kipindi hicho na uthibitisho wa DR ambayo ilikuwa na saini yake aliyoitia baada ya ukaguzi. Shahidi alidai Novemba 14, Inspekta Swila alimfata TAZARA na kumfahamisha kwamba DR inahitajika mahakamani. Alitaja vitu anavyokumbuka vilivyoko nje ya kitabu hicho kuwa ni maandishi ya rangi ya bluu, WEF 01.01.2019 na chini kuna maandishi madogo ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Anadai ndani inasomeka POL/TZR/PR/IR OR RB na kuna jina la ofisa aliyekagua kipindi hicho.

Shahidi aliomba DR hiyo ya Polisi TAZARA, Pugu Road ipokewe kama kielelezo. Upande wa utetezi haukupinga na mahakama ilipokea na kuwa kielelezo namba 3 cha Jamhuri katika kesi ndogo.

Akihojiwa na Wakili wa Utetezi, John Mallya, Maulid alidai jambo linaloshughulikiwa TAZARA ndilo linaloonekana katika DR kama si la TAZARA haliwezi kuonekana na kudai kwamba anafahamu ugaidi ni kosa kubwa na aliwahi kusikia magaidi wameng'oa reli au kufanya ugaidi kwenye treni Pakistan.

Akijibu maswali ya Wakili Fredrick Kihwelo, alidai akipewa maelekezo na kiongozi wa juu anatekeleza lakini Agosti 8, 2020 hakupewa jukumu la kuwahifadhi Kasekwa na Ling'wenya kama anavyodai wakili.

## Jambazi auawa baada kupora mamilioni kituo cha mafuta

**Na Thobias Mwanakatwe**

WATU wawili wanaosadikiwa kuwa majambazi wakiwa na silaha za moto, wamemvamia meneja wa kituo cha kuuza mafuta cha Hike mjini Isongole wilayani Ileje mkoani Songwe na kumpora pesa zaidi ya Sh. milioni 25. Mkuu wa Wilaya ya Ileje ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo, Anna Gidarya, aliiambia Nipashe kwa simu kuwa tukio hilo lilitokea juzi saa 4:00 asubuhi.

Alisema majambazi hao walimvamia meneja wa kituo hicho aliyejulikana kwa jina moja la Matha ambaye alikuwa kwenye bajaji na kumwamuru kutoa mkoba aliokuwa amewekea fedha alizokuwa akizipeleka benki na kumpora.

Alisema majambazi hao ambao walikuwa kwenye pikipiki ambayo haikuwa na namba za usajili, walimvamia meneja huyo maeneo ya Isongole kitongoji cha Chumbageni 'B' jirani na daraja na baada ya kumpora walitokomea kusikojulikana.

Mkuu huyo wa wilaya alisema kufuatia tukio hilo msako mkali wa Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wananchi ulianza mara moja baada ya tukio hilo na kufanikiwa kumkamata na kumuua mmoja kati ya watuhumiwa hao wa ujambazi waliohusika katika uporaji huo.

Mtu huyo aliyefahamika kwa jina la Emili Yeka Mqakayamba (39), alikamatwa na wananchi katika kijiji cha Sange.

Gidarya alisema kuwa mtuhumiwa huyo aliomba lifti katika gari aina ya Fuso kutokana wananchi na Jeshi la Polisi kujipanga na kuweka vizuizi katika njia mbalimbali za kuingia na kutoka Ileje baada ya kulisimamisha gari hilo dereva aliwaeleza viongozi wa kata kuwa kuna mtu wamempakia na wanamtilia shaka ndani ya gari lao.

Alisema baadaye mtu huyo alitolewa katika gari hilo na kumpeleka katika ofisi ya mtendaji wa kijiji kwa ajili ya kumuhoji na kumfanyia upekuzi, na kwamba alidai alitoka kwa mganga na alipoulizwa ni kijiji gani alitoka, alishindwa kukitaja na kuwaomba atoe vielelezo vyake ndani ya begi lake.

Mkuu wa Wilaya alisema walipomruhusu ghafla alitoa bunduki aina ya Ak 47 na kuwaelekezea mtendaji na mgambo waliokuwa wanamuhoji, lakini mmoja kati ya mgambo hao alimrukia na kuishika bunduki hiyo na katika purukushani risasi mbili zilifyatuka ndani ya ofisi.


**COMPLEXE LIMITED**
***LAS VEGAS CASINO***

**EMPLOYMENT OPPORTUNITIES**

Suitable applicants are invited to apply for the following positions:

- **DEALERS; NO EXPERIENCE NEEDED**
- **INSPECTOR/ PIT BOSS; MINIMUM 3 YEARS EXPERIENCE**

**QUALIFICATION**
- Age 20-25 years with minimum height of 5'6"
- Form IV and above, able to communicate in English and Swahili
- Good mathematics skills.

**MODE OF APPLICATION;**
Please submit your application letter accompanied by the following:
- A well detailed Curriculum Vitae (C.V.)
- Copies of relevant Academic Certificates
- Two passport size photographs
- Names of two referees with the inclusion of their mobile numbers
- NIDA

The letter should be addressed to the following address;
**The Manager,**
**Complexe Ltd,**
**P.O. Box 33561,**
**Dar es Salaam.**

The application documents shall be delivered at the reception Desk between 9:00 am and 3:pm, Las Vegas Casino, Upanga. Not later than **03/12/2021.**

***NB: FEMALE CANDIDATES ARE ENCOURAGED TO APPLY.***

116585802



MuCoBa Bank PLC
MUCOBA BANK PLC
P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.
E-Mail: mucoba@mucobatz.com

**TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MBILI (22) WA WANAHISA WA BENKI YA MUCOBA**

Taarifa inatolewa kwa wanahisa kwamba, Mkutano Mkuu wa ishirini na mbili (22) wa Wanahisa utafanyika siku ya Juma mosi tarehe 18 mwezi wa Disemba 2021 katika ukumbi wa MAM –uliopo Mafinga Mjini kuanzia saa tatu kamili asubuhi.

Ajenda za Mkutano zitakua kama ifuatavyo:
1. Utangulizi
2. Kuridhia agenda za mkutano
3. Kuthibitisha Muhtasari wa kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 21 wa Wanahisa uliofanyika tarehe 30. 01.2021
4. Kupokea,kujadili na kuridhia utekelezaji wa yatokanayo na Mkutano Mkuu wa 21 wa Wanahisa uliofanyika tarehe 30.01.2021
5. Kupokea nakupitisha Wajumbe wapya wa Bodi ya Wakurugenzi
6. Kupokea na kujadili taarifa ya Mwenyekiti wa bodi ya Wakurugenzi ya Mwaka 2020.
7. Kupokea na kujadili taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Mwaka ulioshia tarehe 31.12.2020
8. Kupokea na kujadili mapendekezo ya Mkaguzi huru wa hesabu za benki kwa mwaka 2021
9. Kuwasilisha taarifa kuhusu mashauri yahusuyo Benki
10. Kuwasilisha taarifa ya Benki ya mwaka 2020 iliyowasilishwa kwa msajili wa makampuni (BRELA)
11. Kufunga Mkutano.

***Notisi hii imetolewa leo tarehe 25.11.2021***

**Mambo ya kuzingatia**
1. Mwanahisa anayetarajia kuhudhuria Mkutano huu atatakiwa kufanya hivyo kwa gharama zake mwenyewe.
2. Iwapo Mwanahisa anayeruhusiwa kuhudhuria Mkutano na kupiga kura, atashindwa kwa sababu zozote zile kuhudhuria Mkutano, ataruhusiwa kuchagua Mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata na kuzingatia taratibu na katiba ya Kampuni.
3. Nakala za Makabrasha ya Mkutano zitapatikana pia kwenye ofisi yetu kuu iliyopo Mafinga- Iringa.

**KWA AGIZO LA BODI YA WAKURUGENZI**
**PHILIP .R. PHANUEL**
**KATIBU - BODI YA WAKURUGENZI**

216586902

# 907,802 wachaguliwa kidato cha kwanza

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WANAFUNZI 907,802 waliofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi, wakiwamo wasichana 467,967 na wavulana 439,835, wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza Januari, mwakani.

Wanafunzi hao waliofaulu ni sawa na asilimia 81.97 ya wanafunzi waliofanya mtihani huo uliofanyika Septemba, mwaka huu.

Huku idadi hiyo ya wanafunzi wakiwa wamechaguliwa, serikali imewahakikishia wananchi na wadau wa elimu kuwa hakuna mwanafunzi atakayebaki kutokana na ukosefu wa mabweni kwa kuwa serikali imetatua kero hiyo ambayo ilidumu miaka mingi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, alitangaza hayo jana jijini hapa wakati akitoa taarifa ya uchaguzi wa wanafunzi walifaulu na kuchaguliwa kuanza elimu hiyo ya sekondari.

Pia alisema kati ya wanafunzi hao waliofaulu na kupangiwa, wamo wenye mahitaji maalum 2,673 sawa na asilimia 0.29 ambao wavulana ni 1,471 na wasichana 1,202. "Kwa mwaka 2022 kumekuwa na ongezeko la wanafunzi 73,932 sawa na asilimia 8.87 ya wanafunzi waliofaulu ukilinganisha na mwaka 2020 ambapo jumla ya wanafunzi 833,872 walifaulu na kupata sifa ya kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza," alisema.

Waziri alisema mwaka huu kwa mara ya pili uchaguzi wa wanafunzi kujiunga na kidato cha kwanza, umefanyika kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa uchaguzi wa wanafunzi (Students Selection-Management Information System).

"Mfumo huu umesaidia kupunguza muda unaotumika kwenye uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza, kupunguza gharama zinazotumika wakati wa uchaguzi na upangaji wa wanafunzi wa kujiunga na kidato cha kwanza, na kuongeza ufanisi na uwazi katika uchaguzi wa wanafunzi kwa maana ya kuwa kila mwanafunzi anapangwa kwenye shule kulingana na mwongozo wa uchaguzi unavyoelekeza," alisisitiza.

Waziri alisema serikali kupitia TAMISEMI ilifanya maandalizi mapema kuhakikisha wanafunzi wote watakaofaulu mtihani wa kumaliza darasa la saba mwaka huu, wanajiunga na elimu ya sekondari ifikapo Januari, mwakani.

"Kutokana na maandalizi hayo, wanafunzi wote 907,802 waliofaulu na kuchaguliwa wataanza masomo siku moja mara muhula wa masomo utakapoanza. Na katika hatua hii natangaza kuwa muhula wa masomo kwa shule za msingi na sekondari zinazomilikiwa na serikali kwa mwaka 2022 utaanza Januari 17," alisema.

Pia alisema anamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutilia mkazo suala la elimu ya sekondari na kwa mara ya kwanza aliruhusu Sh. bilioni 240 kutumika kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 12,000 nchi nzima.

"Kabla ya uamuzi wa mheshimiwa Rais wa kuongeza vyumba vya madarasa 12,000, shule za serikali za umma zilikuwa na nafasi 430,604 kwa ajili ya kidato cha kwanza ambazo zinaachwa na wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne mwaka 2021.

"Ujenzi huu wa vyumba vipya vya madarasa 12,000 utawezesha upatikanaji wa nafasi za nyongeza 600,000, hivyo kuwa na nafasi 1,030,604 kwa ajili ya kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo 2022. Hii inaleta ziada ya nafasi 122,802 za kidato cha kwanza kulinganisha na wanafunzi waliofaulu ambao ni 907,802," alisema.

Ummy alisema kigezo kikuu kilichotumika kuchagua wanafunzi ni mwanafunzi kufikisha alama za ufaulu kuanzia 121 hadi 300 kati ya alama 300.

"Ninawaagiza wakuu wa shule na watendaji wa elimu katika ngazi zote kuongeza bidii katika usimamizi na ufuatiliaji wa utoaji wa elimu ili kufikia malengo ya elimu yaliyowekwa na serikali"alisisitiza

Alitoa wito kwa wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, viongozi na watendaji wa halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa elimu kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa wanaanza masomo yao Januari bila vikwazo vya aina yoyote ili kutekeleza azma ya serikali ya utoaji wa elimu msingi bila malipo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, mkoani Dar es Salaam jana, wakati akitoa tamko la kituo hicho la kulaani tukio la kikatili linalodaiwa kufanywa na askari polisi wa Kituo cha Polisi Goba Manispaa ya Ubungo mkoani humo, kwa kijana aliyetajwa kwa jina la Issa Kassim. Kushoto ni Mkurugenzi wa Ujengaji Uwezo na Uwajibikaji wa kituo hicho, Felista Mauya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Familia aliyepigwa polisi yaomba msaada kisheria

**Na Christina Mwakangale**

FAMILIA ya Issa Kassim (20), anayedaiwa kujeruhiwa na askari polisi wa kituo cha Goba, mkoani Dar es Salaam, imeomba msaada wa kisheria katika Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ili ndugu yao wapate haki.

Kassim amelazwa chumba cha uangalizi maalumu 'ICU' katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa, Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), na baada ya tukio hilo, Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam lilisema linaendelea na uchunguzi.

Mkurugenzi Mtendaji LHRC, Anna Henga, alisema jana kituo hicho kinalaani tukio hilo na kwamba unahitajika uchunguzi huru, ambao hauhusishi jeshi hilo.

"Jeshi haliwezi kujichunguza lenyewe. Familia ya mtu aliyejeruhiwa wameomba msaada wa kisheria ili kufuatilia hili. Pia, wamedai wanapokea taarifa za vitisho kutoka kwa watu tofauti kuhusu tukio hili," alisema Anna.

Mkurugenzi Ujengaji Uwezo na Uwajibikaji kutoka LHRC, Felista Mauya, alisema ndugu wa familia hiyo walieleza kwamba hali ya ndugu yao si nzuri.

Wiki iliyopita, Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alipotafutwa na gazeti hili kujua uchunguzi wa tukio hilo umefikia wapi, alisema unaendelea. Tukio hilo lilidaiwa kutokea Novemba 10, mwaka huu, kituo cha Polisi Goba, baada ya kijana huyo kukamatwa na askari polisi kwa madai ya wizi wa runinga. Novemba 16, Muliro alisema Jeshi la Polisi limefungua jalada la uchunguzi, huku likiita malalamiko ya ndugu ni mazito."Kijana huyu inadaiwa alikamatwa Novemba 10, mwaka huu kwa tuhuma za wizi wa runinga na baadaye kupigwa huku ikidaiwa ndugu zake walikuwa wakiombwa rushwa ili aachiwe.

"Malalamiko hayo ni mazito, hivyo Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limeshafungua jalada la uchunguzi na mifumo ya kisheria itatumika ili kupata ukweli wa jambo hili na ikibainika ni kweli hatua za kisheria na za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya wahusika. Uchunguzi umeshaanza." Muliro alisema siku hiyo.

Tukio hilo liliibuliwa kupitia taarifa ya ndugu iliyosambaa katika mitandao ya kijamii Novemba 16, ikifichua madai ya ndugu yao kupigwa na askari hadi kulazwa ICU na kudai polisi kutaka fedha ili wamuachie. Sehemu ya taarifa hiyo ilidai kijana huyo alikamatwa na polisi nyumbani kwao Goba, baada ya kuuziwa runinga ya wizi, tukio ambalo ndugu hao walidai mtuhumiwa alilikana kulitenda.

# Tamwa yahimiza kupinga ukatili

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), kimesema ni wakati sahihi kwa wadau kukaa pamoja ili kupanga mikakati mipya ya kumaliza au kupunguza matukio ya ukatili wa kijinsia ambayo yameongezeka.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Dk. Rose Reuben, kupitia taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, kuelekea katika maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, alisema licha ya kuwapo kwa sheria na sera nzuri, lakini ukatili huo bado unaendelea katika jamii hasa kwa watoto na wanawake.

Maadhimisho ya mwaka huu yanabebwa na kaulimbiu: 'Ewe Mwananchi, Pinga Ukatili wa Kijinsia sasa'.

Dk. Reuben alisema maadhimisho hayo yanakuja wakati takwimu za hivi karibuni zikionyesha kukithiri kwa matukio ya ukatili wa kijinsia, ikiwamo ubakaji.

Alisema Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamis, akiwa bungeni alinukuliwa akisema, kati ya Januari hadi Septemba mwaka huu, watoto 6,168 walifanyiwa ukatili wa kijinsia na kati yao, 3,524 walibakwa.

Pia, alisema wanafunzi 1,887 walipata ujauzito katika kipindi hicho.

Alisema takwimu hizo zinamaanisha kwamba, iwapo hatua za haraka hazitachukuliwa, katika kipindi cha mwaka mmoja, zaidi ya watoto 7,000 watakuwa wamebakwa au watoto zaidi ya 12,000 watakuwa wamefanyiwa ukatili.

"Takwimu hizi mpya zinaogofya na kutufanya TAMWA tuone pengine wadau, ikiwamo serikali, wazazi na walezi, tukubaliane na kutamka kuwa; 'Ubakaji sasa ni janga' tunaona ni wakati sahihi wa wadau wa masuala ya ukatili wa kijinsia, kukaa pamoja na kupanga mikakati mipya," alibainisha.

Katika hatua nyingine, TAMWA imeipongeza mahakama kwa kutoa hukumu na kufuatilia kwa ukaribu kesi za ubakaji.

"Ni muhimu kwa taifa, sasa kuendelea kubuni njia mbadala na mpya za kukabiliana na janga hili. Tunaliita janga kwa sababu, watoto 3524 kubakwa si lelemama, bali ni tatizo kubwa katika jamii yetu ambalo linaharibu kabisa mustakabali wa maisha ya kizazi kijacho," alisema.

Dk. Reuben alisema bado wanawake wanaendelea kupokea vipigo, kubakwa, kupewa lugha za kudhalilisha katika jamii zao na kuwafanya kuwa ni kundi linaloomboleza na wakati mwingine kuichukia jinsia yao.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

## OMBI LA KUONESHA NIA USAMBAZAJI WA MAJOPO YA NISHATI YA JUA
## KUMBUKUMBU: 0010007283

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya usambazaji wa majopo ya nishati ya jua katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoa minane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; bomba la mafuta pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

EACOP inahitaji huduma za mtengenezaji mwenye uzoefu na mwenye sifa nzuri kutoa huduma za Usambazaji wa Majopo ya Nishati ya Jua (Sola) na vifaa vyake kulingana na viwango, vipimo na maelezo yaliyotajwa hapa chini:

**VIWANGO:**

Nyenzo, uzalishaji na mkusanyiko wa vifaa vya Umeme wa Jua vitazingatia viwango vifuatavyo:

**VYETI VYA MFUMO WA USIMAMIZI:**

ISO 9001:2015 / Mfumo wa usimamizi wa ubora; ISO 14001:2015 / Viwango vya mfumo wa usimamizi wa mazingira; ISO 45001: 2018 / Viwango vya kimataifa vya afya na usalama kazini, pamoja na marekebisho yake ya hivi punde, isipokuwa kama itabainishwa vinginevyo.

**VYETI VYA BIDHAA:**

IEC 61215 / IEC 61730 / CE / MCS / IN METRO; CEC (US California) / FSEC (US Florida); UL 61730 / IEC 61701 / IEC 62716 ; ISO 9001: kuthibitishwa 2015; ISO 14001: Udhibitisho wa 2015 unaoashiria ufahamu wa mazingira; OHSAS 18001: 2007 iliyoidhinishwa, na marekebisho yake ya hivi punde, isipokuwa ikiwa imebainishwa vinginevyo.

**VIBALI VYA BIDHAA**

Iwe inalingana na IEC 60896; IEC 61427; IS 15549 & IS 16220 Inalingana na JIS C 8702; IEC 62109-1/-2, IEC 62116, EN 61000-6-1/-2/-3/-4, pamoja na marekebisho yake ya hivi karibuni, isipokuwa ikiwa imebainishwa vinginevyo.

**JOPO LA NISHATIYA JUA ITAJUMUISHA VIFUATAVYO:**

- Jopo la nishati ya jua yenye uwezo wa Wati 400.
- Kibadilishaji kigeuzi kinacholingana chenye wigo mpana wa volteji
- 12V – 200 AH betri.
- Chaja controla.

**VIGEZO MUHIMU:**

- MSAMBAZAJI atakuwa na uwezo wa kiwango cha chini cha usambazaji wa Majopo ya nishati ya jua (Sola) 30 na vifaa vyake kwa mwezi ili kukidhi kiwango kitakachohitajika na KAMPUNI. KAMPUNI inategemea kuwa na uhitaji wa angalau majopo ya nishati ya jua (Sola) 220 na vifaa vyake kwa jumla, kwa kiwango kilichoainishwa hapo juu cha Jopo za nishati ya jua (Sola) 30 na vifaa vyake k w a mwezi.
- Hakuna nyenzo au viambatisho vitatumika katika utengenezaji hadi kibali cha awali cha matumizi yake kitolewe na KAMPUNI; wala mabadiliko yoyote katika asili, ubora, aina, na chanzo cha usambazaji hakitafanywa bila ruhusa ya KAMPUNI.
- Kwa ombi, nyaraka za ubora wa bidhaa zinazotolewa zinapaswa kuwasilishwa na mtengenezaji kupitia vyeti vya kufanya kazi kulingana na viwango vinavyotumika. Rekodi zote za matokeo ya vipimo vya ubora zitahifadhiwa na mtengenezaji kwa marejesho yajayo.
- Kabla na baada ya kutoa zabuni kwa Mtengenezaji, KAMPUNI ina haki ya kukagua uwezo wa upimaji na kushuhudia majaribio yaliyofanywa katika kituo cha Maabara cha Mtengenezaji na kutathmini ubora wa bidhaa kulingana na viwango vinavyotumika.
- KAMPUNI itateua mwakilishi kushuhudia majaribio yote yaliyofanywa katika kituo cha maabara cha Mtengenezaji na mwakilishi atawasilisha matokeo yote ya mkandarasi/mzabuni husika & KAMPUNI kwa kujitegemea. KAMPUNI ina haki ya kuidhinisha Bidhaa kulingana na ripoti za majaribio ya ubora kabla ya kupelekwa kwenye eneo la ujenzi.
- Jopo la nishati ya jua na maunzi yake yote yatakuja na dhamana ya vifaa na utengenezaji kwa muda wa miezi 12 tangu tarehe ya kukabidhi.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:
- Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa chini ya upeo wa kazi, kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 10 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au kimataifa
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa:
- Utekelezaji wa programu za aina hiyo kwa viwango vya fedha vya kimataifa kwa ajili ya miradi mikubwa ya miundombinu nchini Tanzania.
- Kusimamia miradi mikubwa na wakandarasi washirika.
- kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali za mitaa na sekta binafsi.
- Wafanyakazi waliopendekezwa kufanya kazi kwenye Mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya ndani, 2017 na ufafanuzi wa Kampuni ya Ndani

**Mawanda haya yanaweza kugawanywa kimkoa au kiutalaam na KAMPUNI inaruhusu Wazabuni kuwasilisha pendekezo kwa ajili ya kipengele kimoja, kadhaa au vyote.**

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11** jioni za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **08 Disemba 2021.** Kichwa cha Habari cha barua pepe ni **0010007283.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

## OMBI LA KUONESHA NIA UTENEGENEZAJI NA USAMBAZAJI WA MADIRISHA
## KUMBUKUMBU: 0010007285

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya utengenezaji na usambazaji wa madirisha katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoa minane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; bomba la mafuta pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

EACOP inahitaji huduma za mtengenezaji mwenye uzoefu na mwenye sifa nzuri kutoa huduma za Utengenezaji na Usambazaji wa Madirisha aina ya Aluminium, kulingana na viwango, vipimo na maelezo yaliyotajwa hapa chini:

**VIWANGO:**

Nyenzo, uzalishaji na uunganishaji wa madirisha ya Aluminium utazingatia viwango BS 4873:2009 – Muongzo wa Madirisha ya Aluminium. Vipimo, pamoja na marekebisho yake ya hivi karibuni, isipokuwa ikiwa imeainishwa vinginevyo.

**VIPIMO:**

Dirisha lenye unene wa 80 x 27 x 1mm Aluminium na yenye ukubwa wa jumla wa 1200 x1200mm juu, inayojumuisha cha mm 5 chenye chandarua chenye nyuzinyuzi 0.25 x 1mm, chuma cha grill chenye ukubwa 25 x 4mm (100x100) uliopakwa rangi na waya wa kahawa. Pamoja na vifungio na na vifaa vyovyote vinavyohusika.

Dirisha lenye unene wa 80 x 27 x 1mm Aluminium na yenye ukubwa wa jumla wa 900 x1200mm juu, inayojumuisha cha mm 5 chenye chandarua chenye nyuzinyuzi 0.25 x 1mm, chuma cha grill chenye ukubwa 25 x 4mm (100x100) uliopakwa rangi na waya wa kahawa. Pamoja na vifungio na na vifaa vyovyote vinavyohusika.

**VIGEZO MUHIMU:**

MSAMBAZAJI atakuwa na uwezo wa kiwango cha chini cha uzalishaji cha madirisha 150 kwa mwezi ili kukidhi kiwango kitakachohitajika na KAMPUNI. KAMPUNI inategemea kuwa na uhitaji wa angalau madirisha 1200 kwa jumla, kwa kiwango kilichoainishwa hapo juu cha madirisha 150 kwa mwezi.

- KAMPUNI inahifadhi haki ya kuthibitisha utengenezaji wa madirisha katika eneo la Mtengenezaji kulingana na mfumo wa usimamizi wa ubora sawasawa na viwango vilivyoainishwa.
- Hakuna nyenzo au viambatisho vitatumika katika utengenezaji hadi kibali cha awali cha matumizi yake kitolewe na KAMPUNI; wala mabadiliko yoyote katika asili, ubora, aina, na aina, chanzo cha usambazaji hakitafanywa bila ruhusa ya KAMPUNI.
- Kwa ombi, nyaraka za ubora wa bidhaa zinazotolewa zinapaswa kuwasilishwa na mtengenezaji kupitia vyeti vya kufanya kazi kulingana na viwango vinavyotumika. Rekodi zote za matokeo ya vipimo vya ubora zitahifadhiwa na mtengenezaji kwa marejesho yajayo.
- Kabla na baada ya kutoa zabuni kwa Mtengenezaji, KAMPUNI ina haki ya kukagua uwezo wa upimaji na kushuhudia majaribio yaliyofanywa katika kituo cha Maabara cha Mtengenezaji kutathmini ubora wa bidhaa kulingana na viwango vinavyotumika.
- KAMPUNI itateua mwakilishi kushuhudia majaribio yote yaliyofanywa katika kituo cha maabara cha Mtengenezaji na mwakilishi atawasilisha matokeo yote ya mkandarasi/mzabuni husika & KAMPUNI kwa kujitegemea. KAMPUNI ina haki ya kuidhinisha Bidhaa kulingana na ripoti za majaribio ya ubora kabla ya kupelekwa kwenye eneo la ujenzi.
- Madirisha na maunzi yake yote yatakuja na dhamana ya vifaa na utengenezaji kwa muda wa miezi 12 tangu tarehe ya kukabidhi.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa chini ya upeo wa kazi, kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 15 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au Kimataifa.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.

**Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa:**

- Utekelezaji wa programu za aina hiyo kwa viwango vya fedha vya kimataifa kwa ajili ya miradi mikubwa ya miundombinu nchini Tanzania.
- Kusimamia miradi mikubwa na wakandarasi washirika.
- kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali za mitaa na sekta binafsi.
- Wafanyakazi waliopendekezwa kufanya kazi kwenye Mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya ndani, 2017 na ufafanuzi wa Kampuni ya Ndani.

**Mawanda haya yanaweza kugawanywa kimkoa au kiutalaam na KAMPUNI inaruhusu Wazabuni kuwasilisha pendekezo kwa ajili ya kipengele kimoja, kadhaa au vyote.**

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11** jioni za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **08 Disemba 2021.** Kichwa cha Habari cha barua pepe ni **0010007285.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Dozi za corona zinaendelea kuletwa, twende kuchanja

**TANZANIA** imeendeleza juhudi za kupambana na tishio la corona, baada ya juzi serikali kupokea chanjo 499,590 za aina ya Pfizer-Biontech kupitia mpango wa COVAX Facility kutoka Marekani ambazo zitakinga Watanzania 249,795 watakaopatiwa dozi hiyo mara mbili.

Lakini tangu kampeni ya chanjo ya ugonjwa huo izinduliwe na Rais Samia Suluhu Hassan mwishoni mwa Julai mwaka huu, nchi imeshapokea jumla ya dozi 1,227,400 za Jensen ambazo zinakinga Watanzania 1,227,400.

Vilevile, dozi 2,578,400 za Sinopharm ambazo zinakinga Watanzania 1,289,200, na juzi zimepokelewa dozi 499,590 za Pfizer, huku Watanzania 1,359,624 wakiwa tayari wamechanjwa.

Tangu kampeni ya chanjo kuzinduliwa, sasa ni karibu miezi minne imepita, na idadi ya waliochanjwa inendelea kuongezeka kutokana na hamasa na elimu kwa umma.

Hapa ttunaona ipo haja ya kuongeza kasi ya uhamasishaji ili watu wajitokeze wengi zaidi kuchanjwa. Ni muhimu jamii ikahamasishwa na kujitokeza kwa wingi, kuchanjwa kwani hatua hiyo itasaidia kupunguza mlipuko wa ugonjwa huo ambao unaelezwa kuwa umeanza kuibuka upya katika nchi za wenzetu.

Tunahimiza umuhimu wa kuchanjwa kutokana na ukweli kwamba, Tanzania siyo kisiwa, bali ni nchi kama nyingine, na inaweza kukumbwa na na ugonjwa huo wakati wowote, hivyo tunashauri uhamasishaji na elimu ya chanjo upewe mkazo.

Mikoa 10 ikiwamo ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Dodoma, Arusha, Mwanza, Ruvuma, Mbeya, Morogoro, Mtwara na Kagera, inatajwa kuwa vinara wa kuchanja watu wengi zaidi.

Ingekuwa ni nafasi nzuri kwa viongozi wa mikoa mingine kujifunza kutoka katika mikoa hiyo, jinsi ambavyo imefanikiwa kuchanja watu wengi ili nao nao wapeleke mbinu hizo mikoani mwao.

Ingawa suala la chanjo ni hiari, lakini kwa kuwa ni tishio kwa usalama wa taifa, tunaona kuwa ipo haja kwa serikali kufika mahali ikapima utendaji wa viongozi wake ngazi za mikoa na wilaya kwa kutumia kigezo cha ufanisi wa chanjo ya corona.

Njia hiyo pia tunadhani inaweza kuongeza kasi ya watu kuachana na elimu ya mitaani inayopingana na chanjo, badala yake watu wanaweza kujitokeza kwa wingi kulinda afya zao dhidi ya ugonjwa huo.

Viongozi na watendaji wa ngazi zote wanaelekezwa kutoa ushirikiano wa hali ya juu ili kuhakikisha wananchi wanahimizwa kwenda vituo vya kutolea huduma hiyo kwa kuwa vita hii ni ya watu wote.

Hivyo wawe ni viongozi wa dini, siasa, asasi za kiraia, tunaona ni vyema washirikiane na serikali katika kuelimisha na kuhamasisha umma wa Watanzania kuona umuhimu wa kuchanjwa.

Kumekuwapo na taarifa kuwa baadhi ya wanaume huwazuia wake zao kwenda vituoni kupata chanjo, kama watu wa aina hiyo wapo, basi tunashauri mamkala husika kufuatilia na kuchukua hatua kwa wahusika.

Tunashauri hivyo, kwa sababu afya ni jambo nyeti, ni vyema mtu akaachwa awe huru kuchanja au kutochanja au aelimishwe aelewe kisha achukue hatua, badala ya kuzuiwa kama ambavyo imewahi kuripotiwa.

Jambo ambalo ni muhimu kuzingatia katika kukabiliana na ugonjwa huo, ni kwamba Tanzania siyo kisiwa hadi isifikiwe na ugonjwa huo, bali ni vyema kuchukua tahadhari kwa kuchanjwa.

Katika Kiswahili, kuna msemo kwamba; 'Kinga ni bora kuliko tiba', hiyo tunashauri umuhimu wa kuzingatia kinga kwa kujitokeza kwa wingi kuchanjwa badala ya kusubiri kupatwa na UVIKO-19.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kunahitajika vituo vya mabasi ili kuwanusuru abiria jua kali, mvua

Na Christina Mwakangale

**USAFIRI** wa umma unatumiwa na wengi, kutoka eneo moja hadi lingine. Hivyo, kunahitajika usalama wa abiria wa maeneo ya kupandia na kushuka vituoni.

Kuwapo vituo vya kupumzika iko wazi ni muhimu kwenye kila sehemu iliyotengwa mahsusi kwa huduma hiyo. Hiyo inawaepusha abiria kupigwa na jua, hususan majira ya mchana ikizingatiwa kipindi hiki ni cha jua kali.

Ni kila mahali mijini na vijijini, watu wanalalamikia kuwapo ongezeko la joto pamoja na ukame. Kwa mujibu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), kuona ongezeko la joto kwenye mikoa mingi mwaka huu, hali inafikia nyuzi joto 36.

Hiyo ni ongezeko la zaidi ya nyuzi 3.5 juu ya wastani wa kawaida imetawala miaka mingi na wataalamu wa afya wanaeleza athari za jua kali kwenye mwili wa binadamu, inajumuisha vipele vya muwasho, ngozi kuungua au hata kusababisha magonjwa ya ngozi ikiwamo saratani.

Kwa usafiri wa jijini Dar es Salaam, wakati abiria anaposubiri usafiri wa umma ni kawaida humchukua hata wastani wa nusu saa kabla ya kufika muda anaoutarajia kuwasili kituoni hapo. Anapokuwa mahali hapo anahitaji kupumzika.

Jambo zuri limefanywa na mamlaka husika kwa kuwa na maeneo mengi ya mwisho wa safari jijini Dar es Salaam, kama vile Makumbusho, Kijitonyama na Ubungo Mawasiliano, kuna vituo vya kupumzika abiria. Katika ujenzi wa barabara mpya, suala la vituo vya kupumzika limezingatiwa.

Kwingineko nako, vituo vya abiria havipo. Hilo linawafanya abiria wasimame juani hapo katika msimu huu mvua hazijaanza na zikianza, kuna suala la kunyeshewa.

Nasema, ulikuwa muda mwafaka kwa sehemu ambazo wameondolewa wajasiriamali, kungejengwa vituo kwa ajili ya abiria, kwa kuwa ni kati ya haki za usafiri wa umma. Huko nyuma huduma hiyo haikuwapo, ila walijitahidi kujibanza katika sehemu hizo.

Nitoe mifano michache, kama vile barabara za Mandela na Uhuru ambako hakuna pa abiria kujihifadhi kituoni, mbadala wao wanaangalia mahali penye mti wajisiriamali au panapokuwapo nyumba jirani.

Si njia hizo tu, barabara za nje ya mji ndio 'usiseme' kukutana na kituo cha abiria ni nadra sana na hata kuwa kama vile imehalalishwa kwa staili yake.

Barabara ya Morogoro, ni mfano mwingime ambako vituo vipo kwenye njia ya mwendokasi pekee. Hapo kunanifanya niendelee kusistiza kwamba, eneo la kupumzika abiria ni muhimu sana. Katika usafiri huu watumiaji wako wa kada tofauti; wazee, watoto, wajawazito na wenye ulemavu.

Vituo vinapokuwapo, vinasaidia kupunguzia abiria hali nyingine inayoonekana kututesa abiria, kupanda na kushuka popote tunapoona kunafaa, hasa gari linapokuwa majonzi panamfaa na kusababisha foleni.

Daktari wa Magonjwa ya Binadamu kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili - Mloganzila, Dk. Milagilo Malombe, anasema hali ya sasa ya joto kali lina athari kubwa kwa afya ya mwanadamu, kama hakuna hatua za haraka zinazochukuliwa.

Anataja kubwa ni kuwataka watu kuzingatia kuupoza mwili kwa maji na kuepuka kukaa muda mrefu kwenye jua kali, ikiwamo kutembea juani muda mrefu bila kujifunika.

Dk. Malombe anasema, katika kipindi kilichopo mtu anapoteza maji mengi mwilini kwa njia ya jasho inayosababishwa na kiwango cha juu cha joto pamoja na maji yanayotoka kwa njia ya mvuke.

Anashauri pia watu waepuke kukaa muda mrefu juani ili kuepusha uwezekano wa kutokwa na jasho jingi hivyo kupoteza maji zaidi na kuumia ngozi.

## HABARI KITAIFA

# Waziri ataka NHC kuwekeza miradi mkakati

**Na Munir Shemweta,**
MISENYI

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amelitaka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuendelea kuwekeza miradi ya kimkakati itakayoliwezesha kujiongezea kipato.

Dk. Mabula alisema hayo juzi wakati akikagua mradi wa jengo la kibiashara la NHC lililiko mpakani mwa Tanzania na Uganda, Mutukula, Wilaya ya Misenyi mkoani Kagera.

Mabula ambaye alikuwa katika ziara ya siku mbili mkoani Kagera, ilichofanya NHC kujenga jengo la kibiashara katika mpaka huo, ndicho serikali inachokitaka pale inapokuwa na taasisi zinazojitegemea katika uendeshaji pia ziwe na njia tofauti za kujiongezea kipato kitakachosaidia kuongeza miradi mingine.

Kwa mujibu wa Dk. Mabuka, mradi wa jengo la biashara Mutukula unatoa fursa kwa wafanyabiashra kutoka nchi jirani ya Uganda kuja Tanzania kununua bidhaa kwa kuwa awali ilikuwa aibu kuona wafanyabiashara wakienda kununua bidhaa katika maduka ya nchi hiyo.

"Ilikuwa aibu tunaenda upande wa pili kununua bidhaa, lakini sasa na wao waje hapa kufanya biashara na hii ni alama tosha kuwa tunaanza kubadilika," alisema Naibu Waziri.

Dk. Mabula aliongeza kuwa ana imani mradi huo ukienda vizuri, eneo lingine linalokusudiwa kujenga maduka, litapata msaada wa fedha za ndani zitakazopatikana kupitia mradi huo.

Aliongeza kuwa ni kweli wafanyabiashara wadogo, maarufu kama machinga, hawawezi kupanga katika jengo la mradi huo, lakini shirika linaweza kujenga maduka kuzunguka jengo hilo yanayoweza kubadilisha sura ya eneo kuonyesha kuwa limepangwa na visiwe viduka visivyoonyesha tofauti kati ya eneo lililopangwa na lisilopangwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, Projestus Tegamaisho, aliishukuru NHC kwa uamuzi wake wa kuwekeza mradi huo katika eneo la Mutukula. Aliiomba NHC kuangalia uwezekano wa kuwekeza mradi kama huo katika mji unaopanuka wa Bunazi wilayani Missenyi.

Meneja wa NHC Mkoa wa Kagera, Maneno Mahenge, alisema mradi huo kwa sasa umefikia asilimia 99 na umetumia asilimia 50 tu ya eneo lake lenye ukubwa wa mita za mraba 7,900.

# NEC yaruhusu kutumia vitambulisho mbadala



**Na Thobias Mwanakatwe,**
NGORONGORO

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imeanza kutoa elimu ya mpigakura katika Jimbo la Ngorongoro mkoani Arusha ambapo imetoa fursa kwa wananchi ambao kadi zao za kupigia kura zimeharibika wataruhusiwa kutumia vitambulisho mbadala.

Elimu hiyo kwa wapigakura inatolewa na maofisa 12 wa tume hiyo katika vijiji,vitongozi na kata vya jimbo hilo ambapo zoezi hilo lilianza Novemba 16, mwaka huu na litahitimishwa Disemba 10 mwaka huu ikiwa ni siku moja kabla ya kupiga kura.

Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu kwa Mpigakura, Monica Mnanka, akizungumza na gazeti hili jana, alisema vitambulisho mbadala viliyoruhusiwa na NEC kutumika katika uchaguzi huo mdogo ni leseni ya udereva, kitambulisho cha uraia kilichotolewa na NIDA na hati ya kusafiria (Passport).

Maofisa hao wa NEC wanawaelimisha wananchi pamoja na mambo mengine, kuwakumbusha tarehe ya kupiga kura, kujitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura na jinsi ya kupiga kura ili kupunguza idadi ya kura zinazoharibika kutokana na baadhi ya wapigakura kutokuwa na uelewa mzuri.

Elimu ya mpiga kura inatolewa kwa wakazi hao kwa njia ya ana kwa ana katika kaya, mikusanyiko mbalimbali kama mikutano ya koo, vitongoji , kata, maeneo zinapofanyika shughuli za kijamii kama biashara, malisho, majosho na vikoba.

"NEC imeamua kuchukua maamuzi ya kuongeza wigo wa utoaji elimu ya mpigakura ili kuhakikisha kuwa wapigakura wanajitokeza kwa wingi kupiga kura na kupunguza idadi ya kura zinazoharibika," alisema mmoja wa maofisa hao.

Walisema elimu ya mpigakura inamwezesha mpigakura na wadau wengine wa uchaguzi kushiriki vyema katika michakato ya uchaguzi.

Uchaguzi mdogo jimbo la Ngorongoro umepangwa kufanyika Disemba 11, mwaka huu ambapo wagombea 11 walioteuliwa na NEC walishaanza kampeni tangu Novemba 16, mwaka huu ambazo zitahitimishwa Disemba 10, mwaka huu.

Uchaguzi huo unafanyika kufuatia kifo cha aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), William Tate Ole Nasha, aliyefariki dunia Septemba 27, mwaka huu. Vyama 11 vya siasa vimesimamisha wagombea, ambao walipitishwa na NEC.


## NOTISI / TANGAZO

**MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD, ,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA (2) | IBRAHIM RASHID IBRAHIM NA HAJI HARAMBE BIBOZE | TUANGOMA-TEMEKE NA VIKINDU-MKURANGA | 10/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | FATUMA RASHIDI MASASI | NYUMBA | FATUMA RASHIDI MASASI | MTAA WA KANUNI KATA YA MABIBO- UBUNGO | 10/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | HURBERT APOLINARY MUSHI | NYUMBA | MWANAISHA IBRAHIM HAJI | ZOMBOKO, CHARAMBE - TEMEKE | 14/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | BETTY BENSON KAGARUKI | NYUMBA | BETTY BENSON KAGARUKI | MTAA WA MSAKUZI – UBUNGO | 16/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | ALLY SHAWEJI OMARY | NYUMBA | ALLY SHAWEJI OMARY | KIBAMBA GOGONI | 22/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | JOYCE MARIJANI MSOFE | NYUMBA | JOYCE MARIJANI MSOFE | KIMARA MICHNGWANI | 14/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | MILLICENT JESSE BUJIKU | NYUMBA | RAMADHANI BARONGO | CHAMANZI MACHIMBO | 16/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | OMARI SAID OMARI | NYUMBA | MIZE MASOUD HASSAN | MIKWAMBE TOANGOMA | 10/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | AMINA OMARY SAIDI | NYUMBA | MOHAMED RAJABU NGULANGWA | VIKINDU | 17/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | SHABANI SELEMANI KIGODI | NYUMBA | SHABANI SELEMAN KIGODI | NYAKASANGWE | 15/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | SIAJALI ELIDADI KAVUYE | NYUMBA | SIAJALI ELIDADI KAVUYE | MUUNGANO -GOBA | 21/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | EMMY ALPHONCE MBILINYI | NYUMBA | MBARAKA SHABANI TWAHA | KITUNDA | 28/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | MKONDA HOUSE OF FOOD | NYUMBA | PAMELA MACHIRA NYITAMBE | KIMANGA SOKOINE | 15/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | MATIKO MATAIGA CHOMETE | KIWANJA | MATIKO MATAIGA CHOMETE | MADALE | 14/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | MWANAHAWA ABDU OMARI | NYUMBA | MWANAHAWA ABDU OMARI | MAPINGA | 20/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | MARYAN GENERAL SUPPLIES | NYUMBA | MARYAN KAPAMA | KIMARA TEMBONI | 21/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MUSSA HUSSEIN MUSSA | NYUMBA | MUSSA HUSSEIN MUSSA | CHAMANZI | 22/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ELIUD SIMON MHEMBU | NYUMBA | ELIUD SIMON MHEMBU | GOBA | 23/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ABUBAKARI JUMA MWAMKOA | NYUMBA | ABUBAKARI JUMA MWAMKOA | KUNDUCHI | 24/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | MUNGAYA NDASKIOY MOLLEL | SHAMBA | BABA LEMOMO KORDUNI | MESERANI-ARUSHA | 10/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | STEVEN PIUS MALISA | NYUMBA | STEVEN PIUS MALISA | KITUNDA | 15/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la Mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwapesayoyotealiyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0765999000/0714939933/0754497396**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

216586702

## Wabunge Kibaha walia msongamano

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WABUNGE wa majimbo ya Kibaha Mjini na Kibaha Vijijini, wameomba Wakala wa Barabara (TANROADS) kutafuta namna ya kuboresha barabara za zamani kutoka Kibaha hadi Mlandizi kupunguza foleni za mara kwa mara katika barabara kuu ya Chalinze - Morogoro.

Wakizungumza wakati wa kikao cha bodi ya barabara kilichofanyika jana mjini hapa, na kuhusisha viongozi mbalimbali wa mkoa, wabunge hao waliomba kuboreshwa kwa barabara hizo ambazo hazijakarabatiwa kwa muda mrefu.

Mbunge wa Kibaha Mjini, Silvestry Koka, alisema wakati serikali ikiendelea na mipango ya ujenzi wa barabara nane, itafutwe namna ya kukarabati barabara ya zamani ili kuondoa foleni za mara kwa mara zinazotokea hasa inapotokea ajali.

"Uandaliwe mkakati wa kujenga kwa kiwango cha changarawe hizi barabara za zamani kwani gari likiharibika katika barabara kuu, magari yanahamia katika barabara ambazo ni za muda mrefu ni mbovu kutokana na kutokarabatiwa kwa muda mrefu," alisema Koka.

Naye Mbunge wa Kibaha Vijijini, Michael Mwakamo, alielezea kipande cha barabara cha Misufini karibu na Mlandizi ambacho kimekuwa kikikumbwa na foleni mara kwa mara.

"Barabara yetu ni nyembamba, hivyo gari likiharibika au ikitokea ajali, foleni inakuwa kubwa na hata katika eneo la Miembe Saba hadi Kongowe kuna wakati foleni inakuwa kubwa. Usipotumia barabara za zamani unakaa muda mrefu katika maeneo hayo," alisema.

Aliiomba serikali kuboresha barabara hizo ili inapotokea dharura isiwaathiri watumiaji ambao ni wa ndani na nje wanaopita katika mkoa.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alisema kero hiyo tayari ameifikisha katika wizara husika na anaendelea kuifuatilia.

"Hii kero naifahamu na nimeishaifikisha panapohusika. Hata mimi inanisumbua mara nyingi, naendelea kuishughulikia ipatiwe ufumbuzi wa haraka," alisema.

Kunenge pia aliagiza TANROADS na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini Tanzania (TARURA) fedha za barabara zinazotengwa zielekezwe kwenye vipaumbele.

Pia aliziagiza taasisi hizo kuwashirikisha wananchi kwenye maeneo ambayo wanatekeleza miradi ya barabara ili kupata historia ya eneo husika kuepuka kuchelewesha miradi kwa vitu ambavyo vinaweza kuepukika.

## KESI YA SABAYA
# Shahidi aeleza sababu kutoa mil. 90/-

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHAHIDI wa 10 wa Jamhuri Francis Mroso (44), katika kesi ya uhujumu uchumi, inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake sita, amedai kwamba alimpatia fedha kiasi cha Sh. milioni 90 kutokana na hofu, baada ya kumwona mfanyabiashara, Cuthbert Swai, kupitia kwenye mitandao ya kijamii akimlalamikia kwenda katika biashara zake akitaka kupatiwa fedha kwa nguvu.

Swai ni mmiliki wa hoteli ya kitalii ya Weruweru River Lodge iliyopo Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro.

Mroso, ambaye ni mfanyabiashara jijini Arusha, alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi, Patricia Kisinda, wakati akiendelea kutoa ushahidi wake.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Tersila Gervas, shahidi huyo, alidai kwamba baada ya kumwona Swai akilalamika kwenye mitandao ya kijamii alipata hofu ambayo ilisababisha kutoa fedha hizo.

Aliieleza mahakama hiyo kwamba hakutoa Sh. milioni 90 kutokana na kutokutoa risiti ya Sh. 100,000 ya matengenezo ya pampu iliyopelekwa na kijana wa Sabaya katika karakana yake kutengenezwa bali alilazimishwa kutoa.

Shahidi huyo, kiongozi huyo wa zamani wa Wilaya ya Hai, alimtishia atampoteza endapo atashindwa kumpatia Sh. milioni 90 alizizohitaji.

Alidai ushahidi pekee unaoweza kuithibitishia mahakama kwamba Januari 22, mwaka huu, alitoa fedha katika Benki ya CRDB tawi la kwa Murombo kiasi cha Sh. milioni 90 ni video ambazo zilirekodiwa na CCTV Camera na Bank Statement.

Katika hatua nyingine mahakama hiyo, ilitupilia mbali pingamizi la mawakili wa utetezi kupinga kupokelewa kwa nyaraka nne kama vielelezo vya ushahidi.

Vielelezo ambavyo vilipingwa kupokelewa mahakamani ni leseni ya biashara ya Francis Mroso, TIN namba ya biashara yake, hati ya usajili wa kampuni na cheti cha usajili wa majina ya kampuni.

Akitoa uamuzi mdogo, Hakimu Kisinda, alitupilia mbali pingamizi hilo kwa kuwa halina mashiko.

Akizungumzia hoja ya vielelezo kuwa siyo halisi, alisema vimekidhi vigezo vya kisheria kupokelewa na sio kama walivyodai mawakili wa utetezi.

Kuhusu hoja ya vielelezo hivyo, vimefikaje kwa shahidi huyo ilhali maofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), alisema kwa sasa katika kesi hiyo Mroso ni shahidi na siyo mshtakiwa.

Awali Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, alipingwa kutopokelewa kwa vielelezo hivyo, akidai kwamba nyaraka mbili za vyeti vya biashara sio vyeti halisi bali ni photokopi.

Mahuna alidai kwamba nyaraka hizo, hazionyeshi zimefikaje kwa shahidi huyo, kwa kuwa awali alidai kwamba TAKUKURU walizichukua kwa ajili ya upelelezi wao katika kesi hiyo.

Akijibu hoja hizo, Wakili Mwandamizi wa serikali, Othmed Mtenga, alidai kwamba shahidi huyo aliomba kutoa nyaraka hizo kwa kuwa anazifahamu na zimewasilishwa mahakamani kwa mujibu wa sheria.

Baada ya malumbano hayo ya hoja, Hakimu Kisinda, aliahirisha kesi hiyo hadi Novemba 24, atakapotoa uamuzi mdogo wa pingamizi hilo.




Meneja wa Kiwanda cha TBL cha Arusha, Raymond Mwaikasu, akizungumza wakati wa uzinduzi wa alama maalumu kwenye barabara kwa ajili ya waendesha pikipiki, katika maeneo sita ya Jiji la Arusha jana, kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), ukiwa ni wa kwanza barani Afrika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi wa MNMA wafundwa

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), Prof. Shadrack Mwakalila, amewataka wanafunzi wa chuo hicho kujiepusha na siasa chuoni hapo na kujielekeza katika mambo ya msingi ya kupata maarifa bora yatakayowasaidia wao na taifa kwa ujumla.

Prof. Mwakalila aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa ukaribisho kwa wanafunzi wapya wa mwaka wa masomo 2021/2022.

Kiongozi huyo pia aliwaeleza wanafunzi kujiepusha na makundi ya uchochezi, migogoro isiyo ya lazima na yale ambayo hayana tija kwao na chuo.

"Mnatakiwa kuwa waadilifu, waaminifu na wazalendo kwa chuo na kwa taifa, someni kwa juhudi na maarifa na mzingatie maelezo yote mnayopewa na walimu na uongozi wa chuo," alisisitiza.

Prof. Mwakalila aliwaeleza wanafunzi hao kuwa wahakikishe wanalipa ada kwa wakati na kujiepusha na tabia ya kughushi na kuazimana vitambulisho.

"Mnatakiwa kujiepusha na tabia ya udanganyifu katika mitihani wakati wote muwapo chuoni hapa na mfahamu elimu mnayoipata hapa ndiyo maisha yenu na nyinyi ni tegemeo la taifa," alisisitiza.

Aliwakumbusha kuwa chuo hicho kinatoa mafunzo katika fani mbalimbali za kitaaluma na mafunzo maalum ya uongozi, maadili, utawala bora, uzalendo na utaifa. Prof. Mwakalila amewataka wahadhiri na wafanyakazi kutoa huduma bora wakati wote.

# WCF yawakumbusha wajibu maofisa utumishi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MFUKO wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umewataka maofisa utumishi na utawala katika halmashauri za mikoa kulinda haki za wafanyakazi kwa kuhakikisha wanafahamu masuala yahusuyo fidia baada ya mfanyakazi kuumia au kuugua kzini.

Kauli hiyo imetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa WCF Dk. John Mduma, kwenye mafunzo ya kuwajengea uwezo maofisa hao kuelewa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi na huduma zitolewazo na mfuko huo.

Alisema kuwa suala la fidia kwa wafanyakazi ni la kisheria baada ya mfuko huo kuanzishwa, hivyo maofisa utumishi na utawala wana wajibu wa kuhakikisha wanatoa taarifa kwa mfuko huo kwa madhila wanayopata wafanyakzi katika sehemu za kazi ili kulipwa fidia.

"Dhumuni kubwa la mafunzo haya ni kuwapa uelewa kuhusu usalama na afya mahala pa kazi, huduma zitolewazo na mfuko na hatua za kufuata wakati wa kuwasilisha madai husasan kuwasilisha madai kwa njia ya (Online Notification System-ONS) inayopatikana kwenye portal.wcf.go.tz," alifafanua Dk. Mduma.

Dk. Mduma alisema dhamira ya serikali ni kuwa na uchumi endelevu ambao utahakikisha Tanzania kubaki katika kundi la nchi zenye uchumi wa kati, hivyo ni muhimu kuwa na wafanyakazi ambao watafanya kazi kwenye usalama na kuleta ufanisi.

"Dhamira hii itawezekana pale ambapo tutakuwa na wafanyakazi wenye uhakika wa usalama wa afya zao katika maeneo yao ya kazi na endapo itatokea bahati mbaya wakapata madhara wakiwa wanafanya kazi basi wawe na uhakika wa kupata fidia stahiki na kwa wakati," alisema mkurugenzi huyo.

Awali Mkurugenzi wa Tiba na Tathmini wa Mfuko huo, Dk. Abdulsalaam Omary, alisema, mafunzo hayo ni ya kwanza kwa kundi la watumishi kutoka TAMISEMI ambao ni maofisa utumishi na utawala.

**Dk. Mduma alisema dhamira ya serikali ni kuwa na uchumi endelevu ambao utahakikisha Tanzania kubaki katika kundi la nchi zenye uchumi wa kati, hivyo ni muhimu kuwa na wafanyakazi ambao watafanya kazi kwenye usalama na kuleta ufanisi.**

# Dawa usafirishaji binadamu yapatikana

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kukabiliana na biashara haramu ya usafirishaji binadamu, serikali imesema kuwa itapeleka wafanyakazi wa majumbani katika nchi ambazo imeingia nazo mikataba na si vinginevyo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Ajira, Kazi, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alibainisha hayo jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa ya mafanikio ya ofisi hiyo kwa waandishi wa habari katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika.

Mhagama alisema mwaka 2018, alipiga marufuku utararibu wa mawakala wa kampuni za ajira kusafirisha wafanyakazi wa majumbani baada ya serikali kugundua kuwa mengi yalikuwa ni bandia.

"Hivi sasa tumetengeneza mwongozo mpya ambao utawabana mawakala wa huduma za ajira na tutahakikisha kuwa tutasafirisha tuu wafanyakazi katika nchi zile ambazo tumeingia nazo mkataba na siyo vinginevyo," alisisitiza Mhagama.

Alisema alipiga marufuku usafirishaji wa wafanyakazi wa kazi za ndani kutokana na kuwapo kwa malalamiko mengi kutoka kwa Watanzania wengi kulalamikia namna ambavyo wamekuwa wakisafirisha kwenda katika nchi za nje.

Aidha, alisema watu waliokuwa wakisafirishwa wengi wao walisafirishwa kwa makubaliano fulani, lakini pindi wanapofika katika eneo husika wanatakiwa kufanya kazi ambazo hawakukubaliana.

"Mwaka 2018, nilipiga marufuku usafirishaji wa wafanyakazi hawa kama kuna mtu ambaye amekwenda katika kipindi hiki baada ya mimi kupiga marufuku basi huyo amekwenda kinyume cha utaratibu hivi sasa tumeingia mkataba na Qatar ambayo ndiyo tutawapelekea wafanyakazi," alisema Mhagama.

Kuhusu malipo ya mafao ya wastaafu mbalimbali nchini, alikiri kuwa suala hilo bali ni kero kwa watumishi waliomaliza muda wao wa utumishi wa umma.

"Ulipaji wa mafao ya wastaafu bado ni changamoto kubwa wengi mafao yanacheleweshwa kutokana na sababu mbalimbali," alisema.

Kutokana na hali hiyo alisema kuwa serikali imeandaa mfumo ambao utasaidia kuondoa malalamiko yatokanayo na sababu mbalimbali ikiwamo ucheleweshaji wa michango kwenye mifuko ya pensheni.

Kuhusu kikokoto cha mafao ya wastaafu, alisema kuwa maelekezo yaliyotolewa na serikali bado yanafanyiwa kazi na majadiliano yakishakamilika taarifa rasmi itatolewa hivyo Watanzania wanapaswa kuendelea kuwa na subira.

Akizungumzi mafanikio ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru alisema imefanikiwa kufanya mabadiliko makubwa ya kiutendaji kwa kutumia mifumo ya TEHAMA, lengo likiwa ni kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuongeza tija katika utendaji wa Idara, Vitengo na Taasisi za Ofisi ya Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla.

Pia alisema ofisi yake imeboresha mfumo wa kielektroniki wa kushughulikia maombi ya vibali vya kazi kwa raia wa kigeni ikiwa ni pamoja na kusimamia, kuboresha na kusanifu mfumo wa vibali.

Alisema, mfumo huo umepunguza muda wa kushughulikia maombi ya kibali kutoka siku za kazi 14 zilizoko kisheria hadi siku 7 kutokana na kupungua kwa hatua za uombaji wa kibali kutoka hatua 33 hadi hatua tatu pekee.

"Aidha mfumo huu umeunganishwa na mfumo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Wakala ya Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na inategemewa taasisi nyingi zaidi za serikali zitaendelea kuunganishwa na mfumo huu," alisema.




Mwenyekiti wa Klabu ya Mbio za Magari ya Iringa, Amjad Khan (kulia), akikabidhi cheti cha shukrani kwa Meneja wa Benki ya Absa Tawi la Iringa, Sheillah Kajuna kwa kutambua mchango wa Absa katika kufanikisha mashindano ya mbio za magari ya Iringa 2021, yaliyofanyika mkoani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakubaliana Tunduru kuwa halmashauri mbili

**Na Stevie chindiye,** TUNDURU

WAJUMBE wa Baraza la Ushauri la Halmashsuri ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, wameridhia halmashauri yao kugawanywa kuwa halmashauri mbili zikiwa ni juhudi za serikali kusogeza huduma kwa jamii.

Kufuatia hali hiyo, wajumbe hao pia wameliomba Baraza la Ushauri la Maendeleo ya Mkoa (RCC) kuridhia na kupitisha mapendekezo yao na kuyapeleka Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya ukamirishaji wa taratibu na kuigawa halmashauri yao.

Hayo yalibainika baada ya majadiliano yaliyofanyika mjini hapa ambapo Mkuu wa Wilaya hiyo, Julius Mtatiro, alihitimisha kwa kuwahoji wajumbe walioshirika katika kikao hicho ambapo asilimia 100 ya wajumbe wote walikubaliana na mapendekezo hayo.

Awali katibu wa kikao hicho, Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Chiza Marando, alisema kuwa ili kuondoa mkanganyiko wa mipaka, mgawanyo huo utafuata mipaka ya majimbo ya Tunduru Kaskazini na Tunduru Kusini.

Marando aliendelea kufafanua kuwa karibu vigezo vinavyohitajika vimetumika ikiwamo uwapo mkubwa wa eneo linalohitajika kwa halmashauri mama na mpya idadi ya kata ambazo zipo 39, tarafa 5.

Katika taarifa hiyo Marando alizitaja tarafa zitakazounda Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru Kusini kuwa ni tarafa za Nalasi, Lukumbule na Namasakara huku Hamashauri ya Wilaya ya Tunduru Kaskazini ni Mlingoti, Matemanga, Nampumgu na Nakapanya.

Katibu Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Kiuma, Daniel Malukuta, aliwataka wataalamu kuzingatia na kukamilisha vigezo vinavyohitajika ili kuepuka kupoteza muda wao na kitegemea huruma ya viongozi wa kitaifa.

# Zuio lafutwa usafirishaji wa bidhaa ghafi za misitu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, ameondoa zuio la usafirishaji bidhaa ghafi za misitu kwa masharti ikiwamo 'veener' na utomvu kutoka miti ya misindano kwenda nje ya nchi mpaka Juni mwakani.

Badala yake ameruhusu kontena 187 zilizopo bandari kusafirishwa na kontena zilizopo nje ya bandari zifuate utaratibu uliowekwa na wizara ili zipate kibali cha kusafirishwa.

Akizungumza kwenye kikao kilichoratibiwa na Baraza la Biashara la Taifa (TNBC) jijini Dar es Salaam, Dk. Ndumbaro amesema lengo la serikali ni kuona sekta ya misitu inatoa mchango stahiki kwenye pato la taifa, na kuwataka wadau kujiandaa na utekelezaji wa maazimio yaliyopitishwa kwenye kikao kilichowakutanisha wadau hao Novemba 15, mwaka huu, wilayani Mafinga.

"Malengo ya serikali ni kuona sekta ya misitu inaleta tija kwa wazalishaji wake. Nyinyi kama wadau hamna budi kujiandaa kutekeleza maagizo ya serikali ili mpate muda wa kujiandaa," alisema Dk. Ndumbaro.

Alisisitiza: "Katika kipindi hiki cha mpito mpaka kufikia Juni mwakani vibali vyote vitatolewa na waziri kwa kufuata masharti yakiwamo kuleta taarifa za kodi, taarifa za haki za wafanyakazi, thamani halisi ya mzigo pamoja na kuwa na mpango kazi wa kampuni wa kuleta mashine haraka."

Aidha, Dk. Ndumbaro aliwataka wafanyabiashara na Watanzania kwa ujumla kukubaliana na mabadiliko ambayo ndiyo msingi wa maendeleo katika jamii yoyote duniani, hivyo amehimiza jamii kuwa katika mtazamo chanya katika kupokea mabadiliko.

"Serikali imefanya utafiti na kujiridhisha kuwa faida inayopatikana katika kusafirisha malighafi ni ndogo, hivyo ili kukuza kipato kupitia sekta ya misitu imeamua kuzuia usafirishaji wa mazao hayo na kuhimiza uwekazaji utakaotoa bidhaa ya mwisho na kwenda sokoni," alisema Dk. Ndumbaro.

Aliongezea kuwa serikali itaendelea kupanua wigo na kutoa fursa zaidi za uwekezaji na ajira nchini kwani kwa kufanya zuio hilo kutachochea uwekezaji wa viwanda vikubwa hapa nchini jambo litakalozalisha ajira na kukuza pato la taifa.

Katibu Mtendaji wa TNBC, Dk. Godwill Wanga, aliwataka wadau hao kuwa na imani na serikali, kwani imefanya maboresho hayo ili sekta hiyo iwe na tija kwa wazalishaji na kuchangia kwenye pato la taifa.

"Kwa muda mrefu sasa sekta ya misitu imeonekana ikitoa mchango mdogo kwenye pato la taifa, kwa kuliona hilo serikali imekuja na maazimio haya ikiwa ni hatua ya kuifanya sekta hii iwe na tija sio tu kwa wazalishaji bali hata kwa uchumi wa nchi," alisema Dk. Wanga.

Naye Mwenyekiti Mwenza wa kikundi kazi cha Misitu TNBC, Ben Sulus, aliwataka wadau hao kubadilika na kuendana na matakwa ya serikali kwa kuwekeza zaidi kwenye kuleta mitambo na kuanzisha viwanda vingi nchini ili uzalishaji ufanyike hapahapa jambo ambalo litatengeneza fursa kubwa za ajira kwa Watanzania.




Ofisa Mauzo wa Kampuni ya kuagiza magari ya Be Forward, Yudathadei Gabriel (kulia), akitoa maelezo kuhusu shughuli mbalimbali wanazofanya kwa baadhi ya wakazi wa Jiji la Arusha, waliotembelea banda lao, wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini humo juzi, ambapo kampuni hiyo ilikuwa moja kati ya wadhamini wa maadhimisho hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC ambana meneja wa TANESCO kisa kuungua transfoma

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti, amemtaka Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani humo kujieleza kwa maandishi sababu za kuungua kwa transfoma mbili na kusababisha kukosekana kwa umeme kwenye baadhi ya maeneo mkoani humo.

Agizo hilo alilitoa jana akiwa katika ziara ya kikazi ya siku moja ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za kupambana na ugonjwa wa Uviko-19 katika Manispaa ya Sumbawanga.

Alisema kuwa kila anapokuwa katika ziara anakutana na maswali kuhusu tatizo la kukatika ovyo kwa umeme, na kwamba wananchi wamekuwa wakihoji kwa nini linawasababishia vikwazo katika shughuli zao na kuwapo kwa hofu ya kuungua vifaa vyao zikiwamo nyumba.

"Nataka Meneja wa TANESCO mkoa unieleze kwa maandishi ni kwanini kumetokea tatizo la kuungua kwa transfoma mbili mara mbili katika kipindi kifupi, na kama suala hilo limekuwa juu ya uwezo wenu ni kwa nini hamjaomba msaada wizarani mpaka sasa?" Alihoji.

Alisema kuwa maeneo mengine ya nchi yamekuwa yakikabiliwa na mgao wa umeme kwa kuwa wanatumia umeme wa gridi ya Taifa, lakini mkoa wa Rukwa unapata umeme kutoka nchi jirani ya Zambia, hivyo suala la umeme wa mgao kutoka gridi ya Taifa haliwagusi wananchi wake.

Katika hatua nyingine, mkuu huyo wa mkoa ameuagiza uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga kukamilisha ujenzi wa zahanati ya Kijiji cha Kankwale iliyoanzwa kujengwa miaka 20 iliyopita, lakini haijakamilika mpaka sasa.

Alisema kuwa mara ya mwisho alipofanya ziara kijijini hapo miezi mitatu iliyopita, aliagiza ujenzi wa zahanati hiyo ukamilike kwani tangu wananchi walipojenga kufikia usawa wa lenta ndio iliishia hapo miaka 20 iliyopita, lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea.

# Wanafunzi 41 wa Rukwa wapata ujauzito miezi 11

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

WANAFUNZI 41 katika shule za msingi na sekondari mkoani Rukwa wamekatisha masomo kutokana na kupata ujauzito katika kipindi cha Januari hadi Novemba 20, mwaka huu. Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti, alieleza kukasirishwa na hali hiyo na kuagiza walimu wanaotuhumiwa kuwapa mimba wanafunzi pamoja na wananchi wengine wachukuliwe hatua za kisheria mara moja.

"Lazima tuongeze mapambano dhidi ya vitendo vya mimba kwa wanafunzi, naagiza ofisa elimu wa mkoa kuchukua hatua za kisheria na kinidhamu kwa walimu wote wanaotuhumiwa kwa makosa hayo pamoja na wananchi wengine hatuwezi kufumbia macho vitendo hivi," alisema.

Alisema kuwa taarifa zinaonyesha kuwa katika Wilaya ya Nkasi, wanafunzi 25 wamepata ujauzito huku wilaya za Kalambo na Sumbawanga kuna wanafunzi wanane kila wilaya wamepata ujauzito, hali inayoonyesha bado jitihada zinahitajika kumaliza tatizo hili.

Katika hatua nyingine, mkuu huyo wa mkoa ameziagiza halmashauri za mkoa wa Rukwa, husan Manispaa ya Sumbawanga kuwatumia vijana wa Skauti kuwabaini wazazi wanaowatelekeza watoto, hali inayochangia ongezeko la watoto wa mitaani.

ama
ALHAMISI NOVEMBA 25, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Mkurugenzi Jiji Dar afunguka siri kung'ara tuzo bora ya afya kimkoa**



Ukurasa 13

Ujue mradi uliomaliza migogoro ardhi sugu iliyoshindikana vijijini



Ukurasa 14

**Mlipuko wa Uviko 19 Ulaya wengi warejea zuio, baadhi chanjo lazima**

UNAIJUA BAROMETA JINSIA?

# TGNP yaanika magumu ya corona na familia kupitia angalizo la SADC

**Na Yasmine Protace**

WASTANI miaka 13 iliyopita, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), ilibuni kipimo cha kufuatilia maendeleo ya kijinsia ndani ya nchi wanachama, ikiwa na viashiria 100; kipimo kiliitwa Barometa ya Kijinsia.

Hapo kuna maeneo saba yanayosimamia viashiria hivyo, ikijumuisha: Uhusiano wa kimapenzi na afya; afya ya vijana; utoaji mimba salama; UKIMWI; matendo hatari; na mambo ya kimapenzi

Mwaka huu, nchi 16 wanachama wa SADC zimekutana kujadili suala hilo, ikiwamo halisi ya chanjo ilivyo. Kimsingi, barometa hiyo inaonyesha ujumbe mzito kwamba sauti ya chaguo haishii katika uadilifu na mwili pekee, bali na haki za wanawake katika jamii.

Hapo kuna mjadala uliozama hata katika afya ya uzazi, ngono salama, afya ya uzazi kijinsia na haki za vijana, utoaji mimba salama, maambukizi ya VVU, ukatili wa kijinsia, ndoa za utotoni na janga jipya la Uviko 19.

Suala hilo la liliangaziwa kwenye barometa hiyo na takwimu zinaonyesha huenda itachukua mwaka mmoja au miwili zaidi.

Katika kipindi cha watu kuamriwa kujifungia maarufu 'lockdown' dhidi ya maradhi hayo katika baadhi ya nchi wanachama, kunatajwa kutawaliwa na utata wa takwimu halisi ya namna Uviko 10 umetawala, hadi kufikia mwaka huu, kwani hakuna takwimu sahihi za wagonjwa kati ya wanawake na wanaume, hali kadhalika vifo vyao.

Waziri wa Afya nchini Malawi, Dk. Patricia Kakiati, anasema hakuna suluhisho sahihi lililofikiwa katika kuweka sawa picha halisi na ya kitakwimu katika uwasilishaji yanayohusu eneo hilo kijinsia, akielekeza jicho mahsusi katika chanjo.

### JICHO LA GEMSAT

Mwenyekiti wa Jinsia Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika Mtandao wa Tanzania (GEMSAT), Dominica Haule, katika uzinduzi wa ripoti ya barometa iliyozinduliwa na TGNP Mtandao, anatamka Uviko 19 imeingia nchini mara ya kwanza mwaka jana.

"Kinamama ni watafutaji. Kipindi cha mwaka jana kulipotangazwa corona na watu tukatakiwa kutulia maeneo yetu. Kwa kweli, kinamama wengi wameharibikiwa biashara zao," anaeleza.

Anafafanua kwamba walifanikiwa kutembelea Dar es Salaam eneo la Slipway, pia Bagamoyo amezuru na kuzungumza na jinsia zote, kinamama na kinababa, ambako kuna kampuni zimekabiliwa 'lockdown; hata wafanyakazi badala ya kupewa mishahara, walipewa posho wakiwa nyumbani.

Dominica anasimulia ziara nyingine katika soko la samaki Feri, Dar es Salaam, ambako amewakuta wakaanga samaki wasio na barakoa na alipowahoji kulikoni hawakuvaa barakoa, alijibiwa kwamba hawakuwa na uwezo wa kununua nyenzo hizo kwa saa nne, hivyo wakaamua kutovaa.

Kuhusu chanjo, ana ushauri watu wajitokeze kupata huduma hiyo na sio kuishia kusikiliza maneno ya watu, ikiendana na elimu kwa umma katika nanma ya kukabiliana na maradhi corona.



Mwanaharakati wa masuala ya kijinsia, Hance Obote, akizungumza jambo katika mkutano wa kijinsia. **PICHA: MTANDAO**

### WANAHARAKATI JINSIA

Mwanaharakati wa masuala ya kijinsia, Hance Obote, kutoka Kituo Cha Taarifa na Maarifa Saranga, anasema mwaka Jana matukio ya ukatili yalifanywa kwa watoto wa kike waliokaa 'lock down' kutoka na maradhi Uviko -19 wakarudi shule na ujauzito, pia baadhi ya familia ziliitumia hayo mazingira kutesa watoto wao.

Anasema, ukatili wa kiuchumi ulijitokeza kutokana na biashara nyingi kufungwa na wenye mali, huku wafanyakazi wakiangukia ugumu wa maisha ya kila siku, hata kukajitokeza athari kwa watoto.

Kuna baadhi ya mashirika yamepunguza wafanyakazi, huku wanafamilia wakiwamo watoto, waliokosa mahitaji ya msingi kutoka kwa wazazi walioathirika kibiashara.

Obote anasema, hali ya watoto kutoenda shule zilipofungwa, ziliwanyima ulinzi dhidi ya ukatoli hasa wa kingono.

Joyce Mkina kutoka Idara ya Nguvu ya Pamoja (TAPO) ya TGNP Mtandao, anfafanua lengo la mkutano wa mwaka 2008 ulijumuisha nchi 26 za SADC kuisaini makubaliano ya itifaki ya kijinsia na kinachofanyika sasa ni tathmini ya 13, ambayo ni ya mwisho kuhusu uzazi kwa wanawake.

AFYA

# Mkurugenzi Jiji Dar afunguka siri kung'ara tuzo bora ya afya kimkoa

- Upanuzi, ujenzi mpya sasa kila kona
- Sh. Mil 750 ya simu yaipa kituo afya

**Na Mwandishi Wetu**

HALMASHAURI ya Jiji la Dar es Salaam, inayoundwa na Wilaya ya Ilala ikiwa na majimbo matatu ya uchaguzi; Ilala, Ukonga na Segerea, ndani yake kuna kata 36, imeongoza kufanya vizuri kwenye eneo la afya.

Inatajwa ni zao la tathmini ya viashiria vya utoaji huduma bora za afya mkoani Dar es Salaam na katika shindano lililofanyika hivi karibuni, ikishirikisha Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam ambazo ni: Manispaa za Temeke, Kinondoni, Kigamboni na Ubungo, tuzo ikiangukia kwa jiji la Dar es Salaam.

Tuzo ya pili ilishirikisha hospitali za rufani za Mkoa Dar es Salaam; Temeke; Mwananyamala ya Kinondoni; na Amana jijini Dar es Salaam, iliyotwaa ushindi.

Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Jumanne Shauri, anaeleza mipango ya kuendelea kutoa huduma bora ya afya kwenye jiji hilo, ikiwamo ujenzi wa zahanati na vituo vya afya pembezoni mwa jiji, ili kurahisisha huduma kwa wananchi.

"Mkutano wa mwaka wa tathimini hiyo ya huduma za afya umekuwa na lengo la kuona hali ya utoaji huduma za afya na kuweka mikakati ya kuboresha zaidi huduma hizo katika hospitali za rufani za Mkoa za Mwananyamala, Temeke na Amana, pamoja na vituo vya afya na zahanati," anasema Shauri.

Anataja vigezo vilivyyoshindanishwa ni: Utoaji huduma bora ya mama na mtoto; utawala na fedha utoaji dawa; maabara; vifaa tiba; mazingira bora; lishe na ustawi wa jamii.

Shauri anasema, utaratibu unaofanywa na Mkoa wa Dar es Salaam wa kuwa na tathmini ya mwaka na kupanga mikakati ya kuboresha utoaji huduma bora, katika sekta ya afya ni chachu kwao kuendelea kufanya vizuri katika utoaji huduma bora kwa wananchi.

Hata hivyo, anazitetea halmashauri zingine za mkoa Dar es Salaam, kwamba zinafanya vizuri, ila kuna maeneo maeneo Jiji la Dar es Salaam, limewazidi.



Hospitali ya Kivule, katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, ambayo ni ishara ya ukombozi katika huduma kwa wananchi waliopo pembezoni mwa jiji hilo. **NA MPIGAPICHA WETU**

### ZAHANATI/ VITUO AFYA

Shauri anasema, kwa kutumia mapato ya ndani, wanajenga zahanati na vituo vya afya vipya, huku ujenzi huo ulioanza kwenye mwaka wa fedha 2019/2020 na mwaka uliopo, mradi huo ni wa zahanati na vituo vya afya vitano.

Anataja zahanati tatu zimeshakamilika na zimeanza kutoa huduma, akizitaja kuwa ni: Lubakaya iliyopo Kata ya Zingiziwa, Luhanga na Mbondole katika kata ya Msongola.

> **Watumishi wa afya jijini Dar es Salaam wako 1,095, ilhali mahitaji halisi ni 1,430, ikimaanisha upungufu wa watumishi 335 au walipo ni asilimia 76 pekee (robo tatu).**

Pia, anavitaja vituo vya afya viwili, Mzinga kinachojengwa katika kata ya Mzinga ambayo ni ghorofa mbili, kikiwa kimekamilika hatua ya boma.

Kingine ni Kituo cha Afya Gulukakwalala, katika kata ya Gongolamboto inayomaliziwa, majengo manne yamekamilika na tano linamaliziwa.

Shauri anataja mradi mingine inayojengwa kwa bajeti ya ndani ni zahanati tano zinazofanyiwa upanuzi kuwa vituo vya afya, ambazo ni Zingiziwa, Kinyerezi na Majohe na Kituo cha Afya Kipunguni.

Shauri anahidi wataendelea kutoa huduma ya afya kwa wazee kama sera ya taifa inavyoelekeza wasio na uwezo kuanzia miaka 60, wanapaswa kutibiwa bure na wawe na dirisha lao la huduma ya dawa, vivyo hivyo huduma ya mama na mtoto.

### FEDHA ZA SIMU

Shauri anasema, serikali hivi sasa kupitia fedha za tozo ya mitandao ya simu, imeshatoa Sh. Milioni 750 kwa ajili ya ujenzi mpya wa Kituo cha Afya Mchikichini; huku kukiwapo upanuzi wa vituo vya afya vya Segerea na, Kiwalani, vikiongezewa majengo,

"Lengo la serikali ni kuboresha huduma za afya pale walipo wananchi, hivyo kwa uwepo wa vituo vya afya wananchi watapata huduma ya upasuaji, utra-sound, x-ray, upimaji na kulazwa," anafafanua Shauri.

### HOSPITALI YA KIVULE

Kupitia Mapato ya Ndani, Mkurugenzi anasema Halmashauri ya Jiji Dar es Salaam, inajenga jengo la ghorofa mbili kwa ajili ya Huduma za haraka na bima ya afya, kwenye Hospitali ya Kivule, ikitengewa Sh. bilioni mbili katika mwaka wa fedha uliopo 2021/2022. Hadi sasa uko hatua ghorofa ya kwanza.

Shauri anasema, nyumba za watumishi zinajengwa kwenye zahanati za Luhanga na Mbondole kila moja nyumba moja, zote zikiwa na uwezo wa kuishi familia mbili zipo katika hatua za umaliziaji.

Anasema zahanati zinazojengwa pembezoni mwa jiji, kwa sasa zinaenda sambamba na nyumba za watumishi, ili kuwapa motisha wahudumu wa afya waishi jirani na maeneo yao ya kazi, pia kuleta tija katika utoaji huduma.

### WAHUDUMU AFYA

Shauri anasema watumishi wa afya jijini Dar es Salaam wako 1,095, ilhali mahitaji halisi ni 1,430, ikimaanisha upungufu wa watumishi 335 au walipo ni asilimia 76 pekee (robo tatu).

Hata hivyo, anafafanua wapo kwenye jitihada za kuomba watumishi wa afya wa kada mbalimbali kila mwaka, kwani bado ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali unaendelea, hali inayofanya kuwapo idadi ya kutosha kuhusu wanaokidhi hitaji hasa madaktari, matabibu wauguzi na wataalamu maabara.

Anatoa takwimu za madaktari waliopo ni nusu, kwa maana 41 kati ya hitaji la 80; matabibu 110, kati ya hitaji la 130; wauguzi waliopo ni 440 na wanaohitajiwa ni 540; hali kadhalika wataalamu maabara 74 kati ya hitaji 90.

### WANUFAIKA WALONGA

Diwani wa Kata ya Mzinga, Job Isaack, anasema Kituo cha Afya Mzinga kitawasaidia wananchi wa kata hiyo na jirani kupata huduma ya afya, kwani huduma zote muhimu zitapatikana hapo.

"Ujenzi wa Kituo cha Afya Mzinga Magole unaendelea, na matarajio ni katika kipindi hiki cha mwaka 2020-2025 kitakuwa kimekamilika kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi wa Kata ya Mzinga na kata jirani, kwani kitakuwa na ghorofa mbili kukidhi huduma zote muhimu kwenye masuala yote ya afya," anaeleza diwani.

Anafafanua kuwa awamu ya kwanza, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeshapeleka jumla Sh. milioni 305, huku kituo kikitengewa bajeti ya Sh. bilioni 1.2 hadi kukamilika kwake.

Mkazi wa kata ya Mzinga, Said Ndembo, anasema kupata Kituo cha Afya Mzinga ni neema kubwa sababu wamekuwa wanadumiwa na kata jirani za Kitunda, pia Buza iliyopo katika Manispaa ya Temeke, hivyo hatua hiyo mpya inawaondolea wananchi, hasa wanawake na watoto.

Ndembo anaushukuru uongozi wa Kata ya Mzinga Isaack, kwa kukaa na Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC) kuwasilisha wazo la kuwapo kituo hicho cha afya.

MAZINGIRA

COFOREST...

# Ujue mradi uliomaliza migogoro ardhi sugu iliyoshindikana vijijini

- Kilichogoma miaka 30, kimewezekana wiki

**Na Christina Haule,** LINDI

MRADI wa Kuhifadhi Misitu kwa Kuwezesha Biashara Endelevu ya Mazao ya Misitu Tanzania (Coforest), umeonyesha ishara ya mafanikio kwa kutatua migogoro ya mipaka iliyodumu kati ya miaka mitano hadi 30 kwenye vijiji vitatu kati ya saba vilivyopo chini yake.

Coforest inaendeshwa na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kwa kushirikiana na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) katika wilaya za Morogoro, Kilosa na Mvomero mkoani Morogoro, Liwale, Ruangwa na Nachingwea mkoani Lindi, pia Kilolo ya mkoa Iringa

Ofisa Mradi kutoka TFCG, Peter Ibrahim, anasema mashirika hayo kwa kushirikiana na wataalamu wa kiserikali ngazi za wilaya, wametatua migogoro iliyodumu muda mrefu katika vijiji vya mradi kwenye wilaya tatu, zikiwamo Ruangwa na Liwale mkoani Lindi.

Anaitaja migogoro ya mipaka ambayo imetatuliwa ni baina ya vijiji Malolo na Ng'alu wilayani Ruangwa, Mkoa wa Lindi, huku simulizi nyingine inaangukia kijiji cha Nambinda, kilichokuwa na historia yake ya mgogoro wilayani Liwale, Lindi tangu mwaka 2009, pale kilipozaliwa kutoka kijiji Mama Mlembwe.

Mgogoro mwingine wilayani Nachingwea ni kati ya vijiji Chimbendenga na Mbondo, ambao unaendelea kushughulikiwa kwa kushirikiana na mamlaka ya wilaya.

Aidha, anataja mgogoro wa kijiji Matuli na Diguzi wilayani Morogoro, uliodumu miaka 30 nao umekwisha kwa sasa.

### SIRI YA MSUGUANO

Ibrahim anasimulia mzizi wa mgogoro vijijini Ng'alu na Malolo uliodumu miaka mitano, walitumia mfumo udadisi wa chimbuko lake na kubaini tafsiri ya ramani kwenye vijiji vyote na uhalisia wa mazingira wanayoishi jamii, ndivyo viliwachanganya.

Anasema katika utatuzi huo, pia wameangalia uhusiano wa vijiji na undugu uliopo kati ya vijiji hivyo viwili, wakabaini mgogoro utaleta mgongano na kuwakosanisha kindugu pande hizo.

Ibrahimu anaeleza wamebaini mfumo wa utawala na tafsiri ya ramani kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ndivyo vilivyogongana, akirejea kitongoji cha Namitende, kimsingi kipo kijijini Malolo, wakati ramani inaonyesha ipo kijijini Ng'alu.



Elida Fundi, Ofisa Sera kutoka MJUMITA akimsikiliza Diwani wa Kata ya Mlembwe, Mohamed Hadid, kwenye msitu wa Hokororo, kijijini Nandimba, wilaya ya Liwale. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE**

> **Ushirikishwaji wa mara kwa mara na vijiji jirani utasaidia, sababu mgogoro hutokea sana kama pale rasilimali inakuwa na thamani kubwa kwa jamii.**

Walitumia fursa hiyo kuwaelewesha wanavijiji usahihi uliopo.

Anasema tafsiri za kisheria zilitumika, ikiwamo Sheria ya Ardhi na Sheria Namba Saba ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982, wakiwaunganisha viongozi wa dini zote mbili, wazee maarufu wanaoyajua maeneo tangu uanzishwaji vijiji hivyo, ndipo wakaleta upatanishi kwa kukubaliana wao wenyewe kimaandishi.

Ibrahim anaeleza shaka yake huko nyuma, kwamba huenda mgogoro huo haukuhusisha makundi yote muhimu ikiwamo katika ngazi husika kama vile vijiji, kata, wilaya na tarafa.

Anasema iwapo wangepata elimu stahiki kuhusiana na madhara ya mgogoro na faida za kuumaliza, kabla ya kukubaliana kwa amani, huenda msuguano uli-oshuhudiwa usingetokea.

Pia, anataja baadhi ya madhara akijumuisha kurudisha nyuma maendeleo vijijini, wakati faida ya maelewano ya kudumu yanairuhusu serikali na hata wadau kuona namna ya kushirikiana nao katika kutatua magumu hayo.

Ofisa huyo anasema, haishii mtazamo katika suala kutatua mgogoro eneo msitu pekee, bali kikuu ni uwapo wa makazi ya kudumu, sambamba na sehemu ya eneo la msitu jirani na usalama wake.

Ushauri wake ni kwamba jamii inapaswa kutambua kuwa popote kwenye rasilimali, ifahamike ni lazima kutakuwa na dalili za migogoro ikiwamo mipaka, kati ya



Ofisa Mawasiliano kutoka TFCG, Betty Luwuge, akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Nandimba wilayani Liwale Mkoa wa Lindi (hawapo pichani).

mtu na mtu au na kijiji, au baina ya vijiji akiweka angalizo kwa mujibu wa uzoefu wao kutatua migogoro.

### MGOGORO MOROGORO

Hapo kuna mgogoro uliodumu miaka 30 kati ya kijiji cha Diguzi na Matuli wilayani Morogoro, tangu mwanzo wake mwaka 1990 wao Coforest waliutatua ndani ya wiki moja.

Imewezekanaje? Ibrahim anafafanua: "Mbinu tuliyotumia ni kuangalia kwa undani zaidi chanzo cha mgogoro na kuangalia wadau muhimu wataohusika katika kutatua mgogoro. Hatutegemei mgogoro kurudi tena hapo."

Hivyo, anawaasa viongozi wa vijiji visivyo na miradi kuangalia namna ya kuepuka migogoro, kwa kukutana na kukaa pamoja kuangalia maslahi mapana ya pande zote, kwani penye migogoro hakuna maendeleo.

Anavipa mbinu vijiji vyenye migogoro ya ardhi, vyema vikakutana kuangalia suluhisho, huku kwa vijiji visivyo na migogoro ya ardhi, nao ni muhimu wakahakiki mipaka na majirani.

"Ushirikishwaji wa mara kwa mara na vijiji jirani utasaidia, sababu mgogoro hutokea sana kama pale rasilimali inakuwa na thamani kubwa kwa jamii," anaeleza.

Ibrahim anaendelea kufafanua:"Kama migogoro haipo kwa sasa ni vyema kuweka kumbukumbu za kutosha ili baadae kusiwe na usumbufu."

Anawashauri wanavijiji sasa waweke vikao vya kila mara na kuviandikia taarifa, ili kuwa na kumbukumbu sahihi inayoweka mbali migogoro ya kugombania rasilimali, hata pale inapotokea, inapunguza hitaji la nguvu kubwa ya viongozi wa serikali usuluhishaji migogoro ya vijiji.

Mzee Maarufu wa kijiji cha Malolo wilayani Ruangwa mkoani hapa, Anastas Maluma (62), anaushukuru mradi huo kufika kijiji kwao mwaka 2019 hata ukamaliza mgogoro wao, wakiwa na imani sasa wanaweza kuanza kunufaika na mazao ya msitu wao wenyewe, manufaa kufikia hata vizazi vyao vijavyo.

### DODOSO LA MAOFISA

Ofisa Mtendaji wa Kata a Malolo, Abdalah Liuba, anasema kupitia mradi huo, yanayotokea Malolo yanabaki historia na sasa vijiji vingine vimetambua uwepo wa miti zaidi ya aina 42 katika maeneo yao, baada ya kupewa elimu.

Pia, anataja kuwapo aina 22 za miti inayoweza kuvunwa kama mbao, hata kuleta faida kwa wavunaji, vijiji na serikali husika.

Ofisa Mawasiliano kutoka TFCG kupitia mradi wa Coforest, Betty Luwuge, anafafanua lengo ni kufikia usimamizi endelevu wa misitu ya asili, utakaoleta mabadiliko ya kiuchumi na kiutawala katika mnyororo wa thamani wa mazao misitu na kuchangia kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Luwuge anasema, kupitia mradi wamekuwa wakielimisha umma kuongeza tija katika ushawishi wa utekelezaji sera za maendeleo ya misitu na mazingira.

Anakumbusha katika utekelezaji wa awali, ndiko walikokumbana na pingamizi za migogoro ya mipaka na kuzitatua kabla ya kuanza kutoa elimu, namna ya kunufaika na usimamizi shirikishi wa mazao ya misitu kwa jamii.

AFYA

# Mlipuko wa Uviko 19 Ulaya wengi warejea zuio, baadhi chanjo lazima

## • Wapingaji waandamana 'hatuzitaki zote'

**Na Mwandishi Wetu**

MAAMBUKIZI ya virusi vya corona yanaongezeka kwenye nchi nyingi za Ulaya kwa kasi, wakati bara hilo linaelekea kwenye kipindi cha majira ya baridi.

Kasi kubwa ya mikasa iko juu zaidi Ulaya Mashariki na kusababisha baadhi ya nchi kufanya uamuzi. Wengi wanatafakari uamuzi iwapo zianzishe tena vizuizi vya kukabiliana na virusi corona kabla ya msimu wa Krismasi na jinsi ya kuwashawishi watu kupata chanjo.

Majadiliano hayo yanatokea huku majirani zao bara Asia, isipokuwa China zinafungua tena sekta ya utalii duniani

Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Hans Kluge, anasema kasi ya maambukizi sasa katika nchi 53 za bara Ulaya inaleta wasiwasi mkubwa, virusi vya corona vinasambaa haraka katika miezi ya baridi wakati watu wanakusanyika nyumbani.

Awali, kiongozi huyo wa WHO, alionya kuna shaka ya kuwa vifo 500,000 vinavyohusiana na COVID-19 ifikapo Februari ijayo. Mkurugenzi Kluge anafafanua:


"Kwa jumla, sasa kuna zaidi ya visa milioni 78 vilivyoripotiwa kwenye nchi za Ulaya, kuliko Asia Kusini na Mashariki, Mediterania Mashariki eneo la Magharibi ya Bahari ya Pasifiki na Afrika kwa pamoja. Kwa mara nyingine tena tuko kwenye kilele cha maambukizi,"

Bara la Ulaya kuna ongezeko la asilimia sita wiki mbili zilizopita kupitia mikasa milioni 1.8; Ujerumani yenye uchumi mkubwa zaidi barani Ulaya imeripoti kuwapo maambukizi mapya 33,949 kwa siku, ikiwa ni ongezeko kubwa kushuhudiwa katika eneo hilo tangu kuzuka maradhi hayo

Pia, kuna nchi kama Russia na Ukraine, janga hilo linazidi kuongezeka, nchini Austria kukiwapo rekodi ya juu zaidi, katika nchi kama Uingereza, maambukizi yameongezeka kwa kiwango cha juu zaidi.

Mataifa ya Hungary na Poland yenye uchumi mkubwa zaidi Ulaya Mashariki, nayo yamerekodi kiwa na mambukizi mapya yaliyovunja rekodi tangu ushuhuda wa Aprili, mwaka huu, hali kama hiyo ikitawala mataifa ya Croatia, Slovenia, Czech na Slovakia.

China, ambako ndiko mzizi wa tatizo, nako kuko katika tahadhari kubwa kwenye bandari za kuingia nchini humo katika juhudi za kupunguza hatari za maambukizi hayo.



Waandamanaji nchini Ujerumani, wakipinga vikwazo dhidi ya mlipuko wa Uviko 19. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Ni Ijumaa iliyopita, Waziri Mkuu wa Austria, Alexander Schallenberg, ametangaza rasmi chanjo dhidi ya virusi vya corona itakuwa ya lazima kuanzia Februari Mosi, mwaka ujao.**

### HATUZA ZA CHANJO

Serikali ya Ujerumani imetangaza vikwazo vya usafiri katika wilaya zake ambako kwa siku saba zilizopita, huku katika baadhi ya majimbo kunaanzishwa vikwazo vya safari kwa ambao hawajapata chanjo, hali kadhalika maeneo kama saluni, vyuoni na vituo vya elimu kwa watu wazima.

Aidha, mkusanyiko wa watu hataruhusiwa na jumla ya watu watano kutoka familia mbili tofauti ndio wataruhusiwa kujumuika pamoja kwa wakati wowote.

Katika matamasha ya kitamaduni na michezo, asilimia 25 tu ya idadi jumla inayokubalika ya mashabiki ndio wataruhusiwa na sheria za kinga zitazingatiwa.

Katika maduka, idadi ya wanaoingia ndani itadhibitiwa: mteja mmoja katika eneo la mita 10 za mraba.

Jimbo la Mashariki mwa Ujerumani, Saxony, limeshatangaza masharti mapya yatakayoanza wiki mbili na nusu zijazo, Desemba 12, kudhibiti maambukizi ya maaradhi Covid 19, ikiwamo kufungwa soko kubwa nchini humo.




Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Ukanda wa Ulaya, Dk. Hans Kluge.

Vilabu, baa, kumbi za mazoezi na au makumbusho pia yatafungwa. Michezo itaruhusiwa kufanyika bila ya mashabiki na marufuku ya kuwa nje usiku kati ya saa nne hadi saa 12.00 asubuhi.

Maofisa Afya wanasema, ongezeko la maambukizi katika jimbo la Saxony huenda ni kutokana na idadi ndogo ya watu waliochanjwa. Ni jimbo lililoko nyuma zaidi, nchini Ujerumani kwa waliopata chanjo.

### AUSTRIA LAZIMA RASMI

Austria imeanza rasmi kukabiliana na wimbi la nne la maambukizo ya virusi vya corona, siku moja baada ya miji kadhaa barani Ulaya kushuhudia maandamano makubwa ya umma.

Ni tangu Jumatatu wiki hii kutekeleza amri ya kuzuia baadhi ya shughuli muhimu za maisha, kukabiliana na idadi ya wanaopoteza maisha kila siku kutokana na COVID-19.

Baadhi ya hospitali zinaonya kwamba uwezo wa vyumba vyao vya wagonjwa mahututi unakaribia kufikia ukomo. Zuio la sasa limepangwa kudumu kwa siku 10, lakini upo uwezekano wa kuongezwa hadi siku 20, watu wanaruhusiwa tu kutoka majumbani wakiwa na sababu za msingi, kama vile kununua vyakula, kumuona daktari na kufanya mazoezi.

Ni Ijumaa iliyopita, Waziri Mkuu wa Austria, Alexander Schallenberg, ametangaza rasmi chanjo dhidi ya virusi vya corona itakuwa ya lazima kuanzia Februari Mosi, mwaka ujao. Ni kama kipindi cha wiki 10 zijazo.

### MAANDAMANO KUPINGA

Barani Ulaya, kulishuhudiwa maandamano ya maelfu ya watu siku ya Jumapili iliyopita, katika baadhi ya nchi wanaopinga uwezekano wa mataifa yao kutangaza marufuku kama hizo zilizoelezwa.

Huko katika makao makuu ya Umoja wa Ulaya (EU), Brussels, Ubelgiji waandamanaji walipaza sauti zao nje kupinga hatua mpya za vizuizi vilivyowekwa ya nchi yao, wakidai wanataka uhuru wao "kuishi bila kubaguliwa kwa sababu ya chanjo ya corona" wakiamini ni uhuru wao wa msingi katika maadili ya magharibi.

"Kuchomwa chanjo kwa kitu kisichofanyiwa majaribio vyema, kutoweza kufanya kazi unapotaka, kuwa utakapo, hayo siyo maadili yetu, huo sio uhuru, hivyo sivyo tunavyoishi, " anatamka mwandamanaji, Eveline Denayer mjini Brussels.

Maandamano kama hayo yamefanyika pia katika miji ya nchi za Ulaya zikiwamo Uholanzi, Denmark na Ujerumani.

***• Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.***





# Bolt yazindua huduma ya usafiri wa bodaboda

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa Jiji la Dodoma wamepanuliwa huduma za usafiri, baada ya Kampuni ya Bolt kuzindua huduma ya usafiri wa kukodi wa bodaboda.

Bolt ni kampuni ya mfumo wa usafiri wa kukodi barani Afrika, ambayo imesema imeanzisha huduma ya bodaboda jijini Dodoma katika jitihada zake za kurahisisha upatikanaji wa huduma za usafiri nchini.

Huduma ya Bolt Boda inawapatia wasafiri njia mbadala ya kusafiri, ikiongeza ukuaji wa huduma za usafiri wa kukodi zinazopatikana sokoni kwa sasa.

Huduma hii vile vile inakusudia kuleta huduma za usafiri za uhakika na za bei nafuu za Bolt karibu na wateja wakati huo huo ikiwa inaimarisha upatikanaji wa huduma zake hapa nchini.

"Tunaendelea kuongeza wigo wa huduma zetu kwa manufaa ya wateja wetu na kuwekeza rasilimali katika huduma zenye ubora ambazo zinakidhi mahitaji ya jamii.

Pikipiki ni moja kati ya njia ya haraka zaidi ya kutoka sehemu moja kwenda nyingine ndani ya jiji la Dodoma, na tunashauku ya kuwapatia wateja wetu njia mbadala na nafuu ya kwenda sehemu mbalimbali ndani ya jiji," alisema Remmy Eseka, Meneja wa Bolt Tanzania.

Alisema uzinduzi wa huduma ya safari ya Bolt Boda unaleta mtandao unaokuwa kwa kasi wa usafiri wa Bolt kwa njia ya bodaboda kwenye miji mitatu nchini ikiwamo Dar es Salaam, Mwanza na Dodoma.

Remmy alisema huduma ya Bolt BODA ni huduma nyingine ya nyongeza katika orodha ya huduma mbalimbali inayotolewa na Bolt, ikiwamo huduma ya Bolt Base na Bolt Lite kwa ajili ya kuhudumia mahitaji ya kipekee ya wasafiri wa Dodoma.

Aliongeza kuwa Kampuni ya Bolt itasajili waendesha bodaboda wenye vitambulisho vya Taifa, leseni ya udereva, cheti cha polisi cha ithibati, leseni ya vyombo vya usafiri LATRA, kadi ya usajili ya gari (usajili wa kibiashara) na bima ya vyombo vya usafiri (kibiashara).

"Biashara yetu kubwa ni kutoa huduma ya usafiri wa uhakika, salama na ya bei nafuu kwa kila mmoja, na tuna shauku ya kufanya huduma ya usafiri iwe rahisi zaidi, ya haraka nchi nzima katika kipindi hiki cha sikukuu," alisema Remmy.

# Madiwani wabariki Ikulu ya Chamwimo kuwa jijini Dodoma

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma limeunga mkono mapendekezo ya serikali ya kuhamisha mipaka ya Ikulu ya Chamwino kuwa sehemu ya jiji hilo.

Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. David Mfupe, alibainisha hayo jana jijini Dodoma wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mchakato huo wa kuhamisha mipaka ya Ikulu ya Chamino kwenda katika Jiji la Dodoma.

Alisema Halmashauri ya Jiji la Dodoma imekuwa katika mchakato wa kutoa maoni juu ya kuhamisha Ikulu kuwa sehemu ya jiji.

"Labda katika hilo ieleweke wazi kuwa hadi sasa hivi tunapoongea asilimia 65 ya eneo la Ikulu lipo Halmashauri ya Jiji la Dodoma na asilimia 35 iliyobaki ipo katika Wilaya ya Chamwino sasa tumepokea maagizo kutoka kwa katibu tawala wa mkoa kupitia mchakato wa kutoa maoni.

"Halmashauri ya Jiji imetoa maoni yake ya kwamba kuhamisha mipaka ya Ikulu kuwa sehemu ya Jiji la Dodoma yapo katika hatua ya mapendekezo na maoni yetu siyo maamuzi yaliyofikiwa,"alisema.

Alisema Halmashauri ya Jiji la Dodoma imeunga mkono kuwa haina tatizo na kata tatu za wilaya ya Chamwino kuwa sehemu ya jiji.

"Tuna kata 41 sasa hivi tukiongezewa kata tatu hayo mambo ya kugawa mipaka ni mchakato inaweza kuwa ni mwanzo wa kuona kuwa kata 44 ni mzigo mkubwa kwa mbunge na halmashauri yenye kata nyingi kuliko nyingine yote nchini.

"Lakini nisisitize kwenu nyinyi wanahabari msije mkatoa picha ambayo siyo sisi tumehusika kutoa mapendekezo na mwamuzi mkubwa ni serikali kuu," alisisitiza.

Kwa upande wao, madiwani wa halmashauri hiyo wameipokeza serikali kwa mapendekezo yake ya kuhamishia eneo hilo la Ikulu kuwa Jiji la Dodoma kutoka Chamwino.

Diwani wa Tambuka Reli Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Juma Mazengo, akizungumza kwa niaba ya madiwani hao aliomba mapendekezo hayo wao kama wawakilishi wa wananchi kutengeneza bajeti ya kuwasaidia kutokana na uhitaji wa maji, miundombinu ya barabara, elimu na afya.

Halmashauri hiyo ya Jiji la Dodoma imekuwa kwenye mchakato huo wa kutoa mapendekezo na maoni juu ya kuhamisha kata tatu ikiwamo ya Chamwino Ikulu, Buigiri na Msanga kuwa sehemu ya jiji hilo.




Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Andrew Komba (katikati), akizungumza wakati wa kufungua mafunzo ya wataalamu wa maabara kutoka mikoa mbalimbali nchini, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Meneja wa Maabara ya Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali Kanda ya Kati, Mussa Kuzumila na Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti wa Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Daniel Ndiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watumiaji kemikali wapewa ushauri

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WATUMIAJI wa kemikali wametakiwa kuzingatia matumizi yake na kuzihifadhi kwenye maeneo salama ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na matumizi mabaya.

Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Andrew Komba, aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya wataalamu wa maabara nchini yaliyoandaliwa na Mamlaka ya maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Kanda ya Kati.

Dk. Komba aliwataka watumiaji wa kemikali wote nchini kuzingatia matumizi sahihi ya bidhaa hizo ili kuepuka madhara yatokanayo na kemikali hizo.

"Kemikali hizi mnazotumia kwenye maeneo yenu ya kazi zina madhara ya moja kwa moja pamoja na kuathiri vizazi vijavyo hivyo nawaomba mkazingatie hayo," alisema.

Aidha, aliyataja madhara mengine ya kemikali hizo zisipohifadhiwa vizuri kuwa ni uharibifu wa mazingira hivyo zinatakiwa kutunzwa kila wakati kwa umakini wa hali ya juu.

Alibainisha kuwa kemikali inatakiwa kuhifadhiwa vizuri pamoja na kuchukuliwa kwa umakini wakati wa kuisafirisha ili kuepuka madhara kwa watu na viumbe wengine.

"Kisheria kemikali inaposafirishwa inatakiwa kusindikizwa na gari lingine linaloashiria kuwa gari imebeba sumu ili kuwatahadharisha watumiaji wa barabara wakati wa kusafirisha," aliongeza.

Kadhalika, alisema sheria ya mazingira namba tatu ya mwaka 2003, inawataka watumiaji wa kemikali kuwa na usajili kwa lengo la kuweka uratibu maalumu wa bidhaa hiyo.

Aidha, aliishukuru Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa serikali kwa kuandaa mafunzo hayo ambayo yatasaidia kupunguza madhara ya kemikali nchini.

Kwa upande wake Meneja wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Kanda ya Kati, Mussa Kuzumila, alisema ofisi hiyo imeandaa mafunzo hayo ya siku nne kwa lengo la kuwajengea uwezo watumiaji wa kemikali nchini.

Alisema mafunzo hayo yanahusisha wataalamu hao kutoka viwanda, watu wa migodi, wataalamu kutoka maabara za Mamlaka za Maji pamoja na walimu wa shule za sekondari.

Aliitaja mikoa iliyoshiriki kwenye mafunzo hayo ni Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Iringa, Singida, Mwanza, Mara, Tabora na Arusha.

Hata hivyo, alisema mafunzo hayo yamekuwa endelevu kwa sababu ya kuhakikisha wanatoa elimu hiyo ili kuepuka madhara ya kemikali.



# KKKT sasa wagombea kiti cha askofu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOGORO wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Konde wa kugombea makao makuu ya Dayosisi, umelipuka upya, baada ya pande mbili zinazovutana kuanza kugombea kiti cha Askofu huku kila upande ukitoa matamko.

Mgogoro huo ulianza kufukuta baada ya Makao Makuu ya Dayosisi hiyo kuhamishwa kutoka Tukuyu wilayani Rungwe kwenda jijini Mbeya ambapo baadhi ya waumini walikuwa wanapinga kuhamishwa kwa makao makuu hayo huku wengine wakikubaliana na uamuzi huo. Kutokana na hali hiyo, baadhi ya waumini wa kanisa hilo hasa wa majimbo ambayo yanapinga kuhamishwa kwa makao makuu waligoma kufanya kazi na Askofu Mkuu wa Dayosisi hiyo, Dk. Edward Mwaikali, huku wakizuia sadaka na michango yote kupelekwa Dayosisi.

Wiki iliyopita Mkuu wa Kanisa la KKKT, Askofu Dk. Fredrick Shoo, akiwa ameongozana na baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama walifika wilayani Rungwe kwa ajili ya kusuluhisha mgogoro huo.

Baada ya mazungumzo yaliyochukua muda mrefu, Askofu Shoo alitangaza kuwa utaratibu wa kuhamisha makao makuu hayo ulikiukwa na akatangaza kuwa yanatakiwa kurejeshwa Rungwe.

Hata hivyo, juzi mgogoro huo ulilipuka upya baada ya waumini kutoka majimbo mbalimbali yanayopinga Makao Makuu ya Dayosisi hiyo kuhamishiwa jijini Mbeya kwenda kuchukua Kiti cha Askofu na kukipeleka Rungwe.

Waumini hao walikusanyika katika Makao Makuu ya Dayosisi hiyo yaliyopo Ushirika wa Ruanda huku wanaomuunga Askofu Mwaikali kuhamishia makao makuu hayo nao wakitoa tamko.

Wakizungumza na waandishi wa habari katika Kanisa la KKKT Ushirika wa Mbeya Mjini juzi, wachungaji zaidi ya 80 wa kanisa hilo kutoka kwenye majimbo matano kati ya saba, walisema mgogoro huo ulitatuliwa na bila kuzingatia mambo ya msingi katika sheria za kanisa hilo.

Mwenyekiti wa wachungaji hao, Mchungaji Nyimbuko Mwambola, alisema msimamo wa wachungaji hao ni hawako tayari Makao Makuu kurejea wilayani Rungwe.

Alisema pamoja na kwamba Askofu Shoo alitangaza kwamba mgogoro huo umekwisha, lakini wao wanauona kama ndio umepamba moto na hawana imani na kamati ya usuluhishi inayoongozwa na Askofu Alex Malasusa wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani.

"Tuliona kwenye vyombo vya habari wanasema mgogoro wetu umekwisha, lakini sisi tunachokiona ni kwamba mgogoro huu kama ni moto ndio kwanza umeshika paa, hatutaruhusu kiti cha Askofu kupelekwa tena Tukuyu kwa sasa," alisema Mwambola.

Alisema Makao Makuu ya Dayosisi hiyo yalihamishwa kwa makubaliano ya vikao halali vya Dayosisi na kwamba vikao hivyo ndivyo vinavyotakiwa kufanya uamuzi wa aina nyingine yoyote ikiwemo kurejesha Makao Makuu Tukuyu. Kwa upande wake, Mchungaji, Judith Kajellali, alisema wao wako tayari kuumaliza mgogoro huo wao wenyewe bila kutegemea nguvu kutoka nje ya Dayosisi hiyo.

Juzi wakati pande hizo mbili zinavutana, Jeshi la Polisi liliimarisha ulinzi kwenye makanisa yote mawili ambapo magari ya jeshi hilo yaliyokuwa yamejaa askari waliojihami kwa silaha za moto, walikuwa wanafanya doria kwenye maeneo yote.



Baadhi ya waumini wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Konde wanaopinga makao makuu ya Dayosisi hiyo kuhamishwa kutoka Wilaya ya Rungwe kwenda Jiji la Mbeya, wakiwa wanaendelea na mapishi katika kanisa hilo, Jimbo la Ruanda jijini humo yalipohamishiwa makao makuu, wakiwa wamepiga kambi kwa zaidi ya siku mbili wakisubiri wapatiwe Kiti cha Askofu, ili warejee nacho Rungwe, hali ambayo upande wa pili unagoma. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Waethiopia mbaroni kwa tuhuma kuingia Tanzania kinyemela

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAHAMIAJI haramu saba raia wa Ethiopia wamekamatwa na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya wakiwa wanazurura mitaani kwa tuhuma za kuingia nchini bila kuwa na vibali vinavyotakiwa.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema wahamiaji hao walikamatwa katika kizuizi cha barabarani cha Iwaga wilayani Mbarali.

Aliwataja wahamiaji hao kuwa ni Izack Feisal (22), Lamato Ibrahim (18), Nasandat Dilen (23), Kelvin Lolanje (30), Andamayo Ababala (20), Zena Gamolo (20) na Jaso Bonkara (19).

Alisema watu hao walikamatwa Novemba 20 saa 12:00 alfajiri wakiwa wanatembea kwa miguu kwenye makazi ya watu wakiwa wanatafuta barabara kuu ili wasafiri kuelekea Afrika Kusini.

"Hakuna mwenyeji wao aliyekamatwa kwenye tukio hilo lakini inaonyesha, kuna uwezekano kwamba walikuwa na mwenyeji wao na alipofika eneo hilo aliamua kuwashusha ili watembee kwa miguu kukwepa kizuizi cha polisi," alisema Kamanda Matei.

Alisema wananchi baada ya kuwaona wahamiaji hao walitoa taarifa Kituo cha Polisi cha Igawa na ndipo maaskari walikwenda kwenye eneo hilo na kuwachukua kwenda nao kituoni.

Kamanda Matei alisema Jeshi hilo linaendelea na taratibu za kuwasiliana na Idara ya Uhamiaji kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria dhidi ya wahamiaji hao.

Aliwataka wananchi wa Mkoa wa Mbeya kuendelea kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo ili kudhibiti vitendo vya uhalifu ndani ya mkoa huo ili shughuli za maendeleo ziendelee kufanyika kwa uhakika na kwa usalama.

# H'mashauri zaagizwa kutenga mikopo ya wenye ulemavu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI zote nchini zimetakiwa kuhakikisha zinatekeleza sheria ya kutenga asilimia mbili kati ya 10 za mapato yake ya ndani kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wajasiriamali wenye ulemavu ili kulisaidia kundi hilo kujiinua kiuchumi.

Agizo hilo lilitolewa jijini Mbeya na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu wa Bunge, Kazi, Ajira na watu wenye Ulemavu, Ummy Nderiananga alipokutana watu wenye ulemavu wa Mkoa wa Mkoa wa Mbeya kuzungumzia kuhusu mambo mbalimbali yanayolihusu kundi hilo.

Alisema Serikali iliamua kuweka utaratibu huo baada ya kugundua kuwa kundi hilo lina uwezo wa kufanya kazi isipokuwa linakabiliwa na ukosefu wa mitaji kama ilivyo kwa makundi mengine maalumu.

Alisema kwa sasa Serikali imeweka utaratibu ambao unawawezesha watu wenye ulemavu kuunda vikundi kuanzia vya watu wawili na kuendelea badala ya utaratibu wa awali ambao ulikuwa unawalazimu kuunda vikundi vya watu wengi zaidi.

"Utaratibu huu ulishapelekwa katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na tayari wakurugenzi wa halmashauri zote nchini mmeshapatiwa maelekezo kwa ajili ya utekelezaji, sasa hakikisheni mnatekeleza," alisema Nderiananga. Alisema kikundi chochote cha watu wenye ulemavu kinachokidhi vigezo vya kukopeshwa ni lazima kipatiwe mkopo na vilelewe ili kuhakikisha vinaendeleza shughuli zao za uzalishaji na kuwa na uwezo wa kurejesha mikopo hiyo.

Akiwasilisha kero za watu wenye ulemavu nchini, Katibu wa Chama cha Watu Wenye Ulemavu (CHAWATA) Mkoa wa Mbeya, Jimmy Ambokile, alisema kundi hilo linakabiliwa na matatizo mengi kwenye jamii ikiwemo kutopewa kipaombele kwenye ajira.

Alisema vilevile kundi hilo linakabiliwa na tatizo la miundombinu isiyo rafiki kwenye taasisi za umma hali ambayo wakati mwingine huwa linasababisha wakose huduma za kijamii.

Alisema baadhi ya majengo ya umma ni ya ghorofa na hayana miundombinu ya kuwasaidia kupanda na mengine hayana njia za kupita kwa watu wanaotumia viti mwendo.

"Tunaomba Serikali itusaidie tupate bima ya afya ili tuweze kutibiwa kirahisi, lakini pia tupewe kipaombele kwenye huduma mbalimbali za kijamii ambazo tunastahili kuzipata kama ilivyo kwa makundi mengine," alisema Ambokile.

Nao baadhi ya wadau waliiomba Serikali kushirikiana na taasisi mbalimbali zisizokuwa za kiserikali kuwasaidia kiuchumi watu wenye ulemavu ili wasiwe wanyonge.

Fedelica Castelana alisema tatizo linalowakabili watu wenye ulemavu nchini hasa watoto ni umasikini wa kipato kwenye familia zao hali ambayo inasababisha wakose malezi bora.

Alisema ili kuhakikisha watoto hao wanapatiwa haki zao za msingi inatakiwa wazazi wao wawezeshwe kiuchumi pamoja na jamii kupewa elimu ya kutosha kuhusu namna ya kuishi na watoto hao ili kuepuka unyanyapaa na kutelekezwa kwa watoto hao.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alipiga marufuku Halmashauri zote za mkoa huo kutoa mikopo ya asilimia 10 itokanayo na mapato ya ndani kwa vikundi vya wajasiliamali bila kuwashirikisha watu wenye ulemavu.

Alisema kabla mikopo hiyo haijatolewa, wakurugenzi wanatakiwa kuhakikisha wanavitafuta vikundi vya watu wenye ulemavu mpaka wavipate ndipo watowe mikopo hiyo huku akiwataka wakuu wa wilaya ya makatibu tawala kufuatilia utekelezaji wake.



# Dk. Mwinyi asisitiza umuhimu kupambana na majanga, maafa

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema hatua za makusudi zinapaswa kuchukuliwa ili kuzuia na kupunguza madhara yatokanayo na maafa, ingawa ni vigumu kuzuilika moja kwa moja.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi katika uzinduzi wa nyumba za maafa katika kijiji cha Nungwi mkoa wa Kaskazini Unguja na Tumbe Mkoa wa Kaskazini Pemba zilizojengwa kwa ajili ya wananchi walioathiriwa na mvua za masika za mwaka 2017. Hafla hiyo ilifanyika Nungwi.

Alisema miongoni mwa hatua zinazopaswa kuchukuliwa ni kuendeleza mipango miji, ambayo inabainisha sehemu za ujenzi wa makazi, sehemu za mabonde zisizopaswa kujengwa, maeneo ya kilimo, maeneo ya ujenzi wa miundombinu ya barabara na maeneo ya huduma za jamii.

"Ni vyema tukahakikisha tunakuwa na 'master plan' ya kila mji tunaoujenga ili kuweka mifumo na taratibu nzuri za kupambana na maafa," alisema Rais Dk. Mwinyi.

Pia alisema ujenzi wa nyumba hizo umelenga kuimarisha maisha ya wananchi baada ya kupatwa na maafa.

Dk. Mwinyi alisema maafa na majanga yamekuwa yakijitokeza katika nchi zote duniani kwa namna mbalimbali na hakuna hata nchi moja iliyo na teknolojia ya kuzuia majanga na maafa kutokea. Alisema hata nchi zilizoendelea hupata taharuki kubwa pale zinapokumbwa na maafa kama vile vimbunga, tsunami, matetemeko ya ardhi, mafuriko na moto.

Rais alisisitiza kwamba yanapotokea majanga na maafa ya aina hiyo, hata nchi zilizoendelea nazo huomba misaada ili kuhami wananchi wake kwa lengo la kujikinga au kupunguza athari za maafa.

Kwa upande wa Zanzibar, Dk. Mwinyi alisema hatua zinaendelea kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kuanzisha kamisheni ya kukabiliana na maafa kwa lengo la kupunguza athari za maafa kwa maisha ya watu na mali zao kwa kuchukua hatua madhubuti za kujikinga, kujitayarisha, kukabiliana na kurudisha hali ya kawaida ya maisha ya wananchi baada ya maafa kutokea.

Naye Kaimu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema familia 54 ambazo zina watu 291 kwa Unguja na Pemba, zinaishi katika vijiji hivyo na wanafunzi wa maandalizi na shule za msingi 277 wanasoma katika vijiji hivyo wakiwamo 151 Nungwi na 126 Tumbe.

Alisema kwa upande wa vituo vya afya tangu vifunguliwe, tayari wananchi 954 wamepatiwa matibabu na huduma mbalimbali za kiafya wakiwamo 230 Tumbe na 724 Nungwi. Pia alisema kuna msikiti ambao unachukua waumini 200 unaohusisha sehemu ya kusalia kinamama.

Waziri Mkuya alisema wananchi waliopata nyumba hizo kutoka mkoa wa Kaskazini Unguja wanatoka katika shehia za Gamba, Mkwajuni, Kidombo na Mkadini na kwa upande wa Tumbe wanatoka katika shehia za Mtemani, Tumbe Mashariki, Tumbe Magharibi, Timba, Kipange na Shumba Viamboni na Wingwi Mapofu na hakuna mtu aliyekuwa hahusiki ambaye amepewa nyumba hizo.

## Kampuni za Uturuki kukarabati barabara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar imetiliana saini na kampuni za ASER na IRIS kutoka Uturuki kutengeneza barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 kwa kiwango cha lami katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Utiaji saini huo ulifanyika jana katika ofisi za wizara hiyo, Kisauni nje ya Mji wa Zanzibar na kushuhudiwa na Waziri wa wizara hiyo, Rahma Kassim Ali. Waliotia saini ni Katibu Mkuu wa Wizara, Amour Hamil Bakari, na mwakilishi wa kampuni za Uturuki, Ertan Murat.

Baada ya utiliaji saini wa mkataba huo Amour alisema mkataba huo utaanza kutumika kipindi kifupi cha kuanza matengenezo kwa barabara hizo za ndani.

Alisema barabara hizo za ndani katika matengenezo yake, zitagharimu Dola milioni 80 na kwamba barabara ambazo sitahusika ni zile ambazo zimo katika mpango maalum wa serikali ya Zanzibar.

Katibu Mkuu alisema kazi hiyo itahusu barabara za Unguja na Pemba ili kuleta ufanisi wa malengo ya serikali ya Zanzibar katika kuzijenga kwa kiwango cha lami.

Amour alisema kabla ya kuanza kwa ujenzi huo, kutafanyika ujenzi mdogo ili kuangalia ubora wa kampuni hizo.

Naye mwakilishi wa Aser na Iris, Murat alisema kwa mujibu wa mkataba huo, kazi hiyo itafanyika kama ilivyokusudiwa.

Alisema watu wa Zanzibar wajenge imani na kampuni hizo ili kufanya kazi yenye ubora zaidi na kudumu kwa muda mrefu kwa sababu kampuni hizo zinafanya kazi kwa uadilifu.



Stesheni Sajini wa Polisi, Mariam Omar Said, akiongoza 'Brass Band', katika uzinduzi wa matokeo ya utafiti ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi 2021, jijini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waandishi watakiwa kusimamia haki za watu wenye ulemavu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kuelekea maadhimisho ya Siku ya Watu Wenye Ulemavu Duniani Desemba 3, mwaka huu, vyombo vya habari vimetakiwa kuwa mstari wa mbele katika kupigania haki za watu wenye ulemavu.

Hayo yalisemwa jana mjini hapa na Mwenyekiti wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar, Ali Omar Makame, wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema vyombo vya habari vina nafasi kubwa ya kusukuma mbele maendeleo ya watu wenye ulemavu ikizingatiwa kuwa ni wadau wakubwa wa maendeleo.

Makame alisema watu wenye ulemavu wanakabiliwa na changamoto nyingi kutokana na kutengwa na jamii kielimu, kiafya, kijamii na kiuchumi ndiyo maana walikuwa duni katika kupata huduma muhimu.

Alivitaka vyombo vya habari kuwasaidia watu wenye ulemavu ili kupata haki zao zinazostahili kama watu wengine wasio na ulemavu.

Alisema ni vyema kuwe na miundombinu rafiki katika kupata haki zao za msingi ikiwamo haki ya elimu na kupiga hatua zaidi za kimaendeleo.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Salum Mkuya, alisema katika kuimarisha zaidi usimamizi wa fursa na haki za watu wenye ulemavu, wizara yake kupitia idara ya watu wenye ulemavu imefanya mapitio ya awali ya Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na. 9 ya mwaka 2006 na rasimu hiyo inaendelea kupata maoni ya wadau.

Alisema marekebisho ya sheria hiyo yataongeza ufanisi katika utoaji wa haki na fursa kwa watu wenye ulemavu pamoja na kuimarisha masuala ya makundi ya watu hao katika sekta mbalimbali zinazogusa maisha yao, hivyo kuongeza kasi ya kuwafanya waishi maisha bora zaidi.

"Ili kuhamasisha uelewa juu ya haki na fursa za watu wenye ulemavu, ofisi yangu inashirikiana na taasisi zisizo za kiserikali 10 kuhamasisha marekebisho ya miundombinu ya majengo hususan ya serikali kwa ajili ya kufikika kwa urahisi zaidi," alisema.

Pia alisema miundombinu ya barabara inayoendelea kurekebishwa, imesaidia kwa kiasi kikubwa kwa watu wenye ulemavu kupunguza vihatarishi vilivyokuwa vikitokea awali katika barabara.

Waziri huyo alisema kuna changamoto kwa baadhi ya watu wenye ulemavu kushindwa kupata matibabu kutokana na kutomudu gharama za matibabu pamoja na uhaba wa dawa hospitalini kwa wenye ulemavu mchanganyiko.

Zanzibar inakisiwa kuwa na watu wenye ulemavu 74,500 lakini mfumo wa kidigitali wa Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu umesajili watu 8,488 wenye ulemavu wakiwamo wanawake 4,043 na wanaume ni 4,445.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**GEORGE J MALOWA** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne index namba **S1802-0088** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia secondary ya BWERI mwaka 2011, na certificate yenye namba **CCIT/MS5/3402/MZB/T.12** iliyotolewa na UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM COMPUTING CENTRE mwaka 2013, na cheti cha diploma kozi ya COMPUTING AND INFORMATION TECHNOLOGY kilichotolewa na chuo cha UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM COMPUTING CENTRE namba **DCIT/MS5/2768/MZB/T.13 mwaka 2015**
Polisi taarifa **MAR/MUS/RB/77544/2021**

116584302

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**DEBORA SHAIBU NYIKA** anatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 584 CMR.** Engine namba **AK4AL44M2845.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MKB/RB/284/2021.**

116585902

**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZAMIA**

**TEMEKE HIGH COURT SUB-REGISTRY**
**(ONE STOP JUICIAL CENTRE)**
**AT TEMEKE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 31 OF 2021**

**In the matter of the estate of the late ALOYCE WENCESLAUS MAYO**

**And in the matter of application for the letter of administration of the late ALOYCE WENCESLAUS MAYO DECEASED OF DAR ES SALAAM**

**By FATINA SENZOTA SAIDI AND FRANK ALOYCE MAYO**

**GENERAL CITATION**
**(rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the the proceeding if they think fit before the grant letters of administration is made to the above named petitioner
Objections to the grant should be filed on or before the 2nd day of december,2021
Dated at this 17th day of November,2021

DEPUTY REGISTRAR

116585702

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLICK OF TANZANIA**

**IN THE DISTRICT REGISTRY OF BUKOBA**
**AT BUKOBA**

**LAND REVISION NO 68/2020**
**(Arising from MULEBA DLHT APPLICATION NO 63/2015)**

**WINCHSLAUS ABEL& 2 OTHERS..................................APPELLANT**

**VERSUS**

**CYRIACUS RAIMOND..................................RESPONDENT**

**TO,1.CYRIACUS RAIMOND**

**RE:NOTICE FOR DATE OF MENTION**

Whereas the above mentioned appellant has lodged a case registered as Land Case Appeal NO 68/2020 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.
Take notice that the above said case has been scheduled for mention on 30 day of November,2021 at 09.00 am before Hon A.MWENDA J.You are authorized to appear in person or through your Advocate.
Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case will proceed in your absence.
Given under my hand and seal of the court this 25,day of October,2021

J.M. MINDE
DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
BUKOBA

116585402

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ELIZABETH STEPHANO NYARI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA FUNCARGO** yenye namba za usajili **T 957 CUG** chasis namba **NCP200279457** engine namba **2NZ2705200,** yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **KW/RB/5602/2021**

116585202

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Kihonda**
**Wilaya ya Morogoro**
**Mkoa wa Morogoro**

**Usimamizi wa Mirathi Na 02/2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**

**MAREHEMU RAMADHANI JOHN MHANDO WA KARUME B. KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ELIZABETH RAMADHANI MHANDO TANGAZO**

**(Kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja kuhudhuria shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 20 Mwezi 12 Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo .

**Zingatia**

Endapo Kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

- Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

Imetolewa Leo 23 Mwezi 11 Mwaka 2021

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO BOMA
MOROGORO

116587202

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**SIRAJI MAGOGO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 974 BGM** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH/RB/562/2021**

116587102

**KUSAFIRISHA MZIGO**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UJENZI,UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**TANGAZO**

Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAPILI tarehe **28/11/2021.**kampuni ya **SAID SALIM BAKHRESA&COMPANY LIMITED**. itasafirisha mizigo yake yenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **BAGAMOYO SUGAR** kupitia **BAGAMOYO ROAD.**

1.Gari hizo zenye namba za usajili na vipimo vyake

a) **T 346 DRJ/T 332 DRN UREFU 20 UPANA 4.7 KIMO 4.6**
b) **T 121 DNB/T 324 DRN UREFU 20 UPANA 4.7 KIMO 4.6**

Gari hilo linatoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **BAGAMOYO SUGAR** kupitia BAGAMOYO ROAD.gari zitasafiri muda wa mchana tu(kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

116586402

## KUPOTEA KWA HATI YA NYUMBA

**NDUGU SALIMU AZUBERY BIGAMBO** anatangaza kupotelewa na hati ya Nyumba **No.04 Plot 5 Block 55 Area A-JIJINI DODOMA.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba **DOD/DOD/RB/546765/2021**

116586302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TARIQ ABUSHIRI KILUNGO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 951 CDS – SUBARU IMPREZZA.** Chassis namba **GG2042004.** Engine namba **EJ15B885374** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/557732/2021.**

116586202

**MAJEMBE AUCTION MART LTD**
**(VIJANA WA KAZI)**

## TANGAZO LA MNADA WA GARI

Kwa niaba ya **K-FINANCE LTD** tutauza kwa mnada wa hadhara gari la mdaiwa anayetajwa hapo chini.
Mahali: Yard ya Majembe Auction Mart, Dar es salaam, Mwananyamala.

| JINA LA MDAIWA | DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|
| Agnes Mutiganzi | Suzuki Vitara – T 111 DRX | Jumatano 01/12/2021 Kuanzia saa 5:00 asubuhi. |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalipa hela yote iliyoafikiwa kwenye mnada.
2. Gharama za kubadilisha umiliki ni za mnunuzi
3. Kwa maelezo Zaidi wasiliana nasi kwa simu namba **0715980025, 0738165605, 0738165606.**

116586802

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 60 OF 2021**

**In the Matter of the Estate of the Late MICHAEL MWAISOKOLA KASITILA**

**BY 1. YOHANA MICHAEL KASITILA**
**2. ........................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 7 day of 12....2021

Dated at Morogoro this 23 day of NOVEMBER.....2021

RESIDENT MAGISTRATE

116587302

***NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA***

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Bilioni 1.6/- kujenga madarasa Namtumbo

**Na Gideon Mwakanosya,** NAMTUMBO

SERIKALI imeipatia Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma Sh. bilioni 1.6 kujenga vyumba 86 vya madarasa.

Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Dk. Julius Ningu, akizungumza katika mradi wa ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika Shule ya Sekondari Nasuli mjini Namtumbo, alisema jana kuwa theluthi moja ya madarasa 86 imefikia hatua ya lenta na ujenzi unaendelea kwa kasi.

"Hadi kufikia Jumamosi ya wiki hii, majengo yote ya vyumba vya madarasa 86 katika Wilaya ya Namtumbo yatakuwa yameshafungwa lenta na kujiandaa kuezeka wiki inayofuata,'' alisema.

Dk. Ningu alisema mifumo mizuri ya usimamizi wa madarasa hayo kwa kuwatumia wenyeviti wa kamati za ujenzi wananchi wenyewe kutoka maeneo ya mradi, imesababisha utekelezaji wa mradi kufanyika ndani ya wakati.

Alisema kutokana na maelekezo ya serikali kukamilisha mradi wa madarasa kwa wakati, walijiwekea utaratibu wa kufanya ujenzi kwa awamu kuanzia msingi, boma, kufunga lenta na kuezeka na kwamba awamu za ujenzi ziliwekwa kwa muda maalum wa siku nne hadi saba katika kila hatua hali iliyosababisha mradi kwenda kwa kasi kubwa.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Nasuli, Dafrosa Chilumba, alishukuru serikali kwa mradi wa vyumba vitatu vya madarasa ambao alisema utapunguza uhaba wa vyumba vya madarasa katika shule hiyo.

Chilumba alisema shule hiyo ina wanafunzi 1,211 wa kidato cha kwanza hadi cha sita wanaosoma katika madarasa 22 na kwamba shule hiyo ilikuwa na upungufu wa vyumba vinane, hivyo kuongezeka kwa vyumba vitatu kumepunguza uhaba wa madarasa.

Hadija Khamis, mwanafunzi wa kidato cha tano katika shule hiyo, aliipongeza serikali kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa ambavyo alisema vitapunguza msongamano wa wanafunzi madarasani, hivyo walimu na wanafunzi kushiriki vyema katika kufundisha na kujifunza.

Mkoa wa Ruvuma umepokea Sh. bilioni 12.7 sawa na asilimia 2.4 ya Sh. bilioni 635.68 ambazo zimeidhinishwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa ajili ya uboreshaji wa sekta za afya, elimu na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

# WMA yataka wananchi kutoa taarifa kuhusu upunjaji vipimo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Vipimo (WMA), umewataka Watanzania kutoa taarifa kwenye ofisi zake kwa kutumia namba za simu za bure kila wanapohisi kupunjwa vipimo na baadhi ya wafanyabiashara.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Stela Kahwa, alitoa rai hiyo jana wakati akizungumza kwenye uhakiki wa mizani unaofanywa kila mwaka kwa nchi nzima.

"Sisi tunawaambia wananchi kwamba wakati wowote wanapokuwa na malalamiko, mapendekezo wasisite kuwasiliana na sisi kupitia namba ya bure tunapatikana nchi nzima. Lazima wafahamu kwamba WMA iko kwa ajili yao 0800110097 na iko nchi nzima," alisema

Alisema wanapima na kuhakiki vipimo vinavyotumiwa na maofisa wake na kazi hiyo ndiyo inawahakikishia kuwa vipimo vinavyotumiwa na maofisa wake viko sahihi.

Kahwa alisema vipimo vinavyotumiwa na maofisa vipimo vinakaguliwa kila mwaka mara moja na vinapoonekana vimepata hitilafu vinarekebishwa.

Alisema katika ofisi ya WMA Ilala, Dar es Salaam, wana maabara ambayo inahifahi vipimo vyenye usahihi wa hali ya juu ambavyo hulinganishwa na vipimo vya nchi nzima na vile vya kimataifa.

"Hii inamaanisha nini, ni kwamba kilo moja ya Tanzania iwe sawa na kilo moja ya Ufaransa, China au India, hivyo kupitia shirika la vipimo duniani kuna namna ambavyo vipimo vyote vya kila nchi vinapimwa na vinalinganishwa na vile vinavyotumika ndani," alisema.

Mtendaji huyo mkuu alisema kwa hapa nchini kila mwaka vipimo vyote lazima vikaguliwe na kuwekwa muhuri mpya na maofisa vipimo wa WMA

Alisema wanaandaa vipimo hivyo kwaajili ya kuhakiki vipimo kwa mwaka 2022 ambapo vipimo vyote ikiwemo pampu mawe na mizani vitapimwa upya na kuwekewa alama za kuthibitisha kwamba zimehakikiwa.

Kahwa alisema wameita maofisa vipimo wote wa nchi nzima kwajili ya kuhakikisha vipimo vyote wanavyotumiwa vinahakikiwa kwajili ya mwaka ujao.



Maofisa wa Wakala wa Vipimo (WMA), wakihakiki mzani unaotumika kuhakiki mawe makubwa ya kilo 500 katika zoezi la uhakiki wa vitendea kazi vya WMA mikoa yote ya Tanzania Bara. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# RC Lindi awapigia chapuo wanawake uhifadhi misitu

**Na Christina Haule, LINDI**

MKUU wa Mkoa wa Lindi, Zainabu Telack, amewahimiza wanawake kujikita katika shughuli za maendeleo ikiwamo usimamizi shirikishi wa misitu ya jamii (USMJ), ili kuona tija ya mazao ya misitu kama ilivyo kwa wanaume na kukamilisha dhana ya jinsia.

Telack alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea vijiji vya mradi wa kuhifadhi misitu kwa kuwezesha biashara endelevu ya mazao ya misitu Tanzania (CoForEST) unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Uswisi (SDC).

Alisema wako wanawake wanaoonekana kwa uchache katika shughuli za maendeleo hasa uzalishaji wa korosho lakini si suala la uhifadhi kwenye mazao ya misitu.

Wanawake wa Lindi, alisema wako kwenye shughuli ya kuokota korosho, kubangua na uuzaji samaki pekee lakini hawako kwenye suala la umiliki wa mashamba wakati ni halali yao na ni jambo la kuwaingizia kipato kingi kama ilivyo kwa wanaume.

Hivyo aliwahimiza wanawake hao kujikita katika shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwamo ukataji miti na uchomaji mkaa kitaalamu kama wanavyofundishwa na wadau wa misitu, hivyo kuona faida za uhifadhi wa misitu.

Naye Mtafiti na mtaalamu wa masuala ya jinsia kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. John Jeckoniah, alisema suala la mgawanyo wa majukumu katika shughuli mbalimbali za kijamii zikiwamo za uhifadhi wa misitu, zinafaa kuzingatiwa ili makundi mbalimbali ya kijamii yafikie fursa za rasilimali za misitu ya asili iliyopo.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Malolo wilayani Ruangwa, Mohamed Abdalah, alisema kwa sasa wananchi wa eneo hilo wana hamasa kubwa ya kuinua uchumi wao baada ya kujua thamani ya msitu na mstumizi bora ya ardhi. Pia alisema wameanza kuhamasika na shughuli za uhifadhi.

Mmoja wa wajumbe wa Kamati ya Maliasili kutoka Kijiji cha Malolo, Hilda Mwambe, aliyashukuru mashirika ya TFCG na MJUMITA kwa kuwajengea uwezo wa kujiamini na kusimama kuzungumza mbele za watu sambamba na kuanza kufanya shughuli za USMJ kwa maendeleo ya familia zao.

Alisema licha ya changamoto wanazopata kutoka kwa baadhi ya waume zao kuwazuia kufanya shughuli hizo kwa madai kuwa zinatumia muda mwingi msituni, wamekuwa wakiungwa mkono na waume hao baada ya kuelimishwa.

# KIVUMBI KUTIMKA IJUMAA NUSU FAINALI UMOJA CUP 2021

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi wa michuano ya Umoja Cup inayoendelea wilayani Rorya mkoa wa Mara, Shirati Mji FC, wamefanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali baada ya juzi, Jumanne kuichapa timu kongwe ya Michire, Rifa FC kwa bao 1-0 katika mechi kali ya robo fainali iliyopigwa Uwanja wa Maji Sota.

**Kwa matokeo hayo, sasa Shirati Mji katika hatua nusu fainali, itashuka dimbani Jumapili wiki hii kuvaana na Wanamaji FC ambao Jumapili iliyopita walitoa Magamaga FC katika mechi nyingine ya robo fainali.**

Katika mechi hiyo ya juzi, licha Rifa fc kuwa na kipa wao mahiri maarufu kama Power, haikuweza kuhimili ubora wa Shirati Mji kwenye mchezo huo uliovutia mashabiki wengi wa soka wilayani Rorya na vitongoji vyake.

Finias Frank, ndiye aliyeihakikishia Shirati Mji kutinga nusu fainali baada ya kuifungia timu yake bao pekee dakika ya 69, katika mchezo huo uliochezeshwa na mwamuzi wa ngazi ya Taifa, Francis Kembo Azaria.

Katika mchezo mwingine wa robo fainali uliopigwa Ijumaa iliyopita kwenye Uwanja wa Maji Sota, Menonnite iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Masonga FC, hivyo hatua ya nusu fainali Jumamosi, itakutana na Kirengo FC iliyoitoa Watumishi FC kwa bao 1-0.

Mabao ya Menonnite FC katika mechi hiyo yaliyofungwa na Joel Joel na Eliya Boaz huku bao pekee la Masonga fc likifungwa na John Amza.

Kuelekea hatua hiyo ya nusu fainali Jumamosi na Jumapili wiki hii, Mwenyekti wa mashindano hayo, Ochieng Melly, amesema wataimarisha ulinzi zaidi kwa sababu mechi zote mbili ni kama fainali kutokana na michuano hiyo kuhudhuriwa na mashabiki wengi tangu imeanza.

Alisema mechi ya kutafuta mshindi wa tatu itapigwa Desemba 3, kabla ya fainali ya michuano hiyo ambayo imekuwa ikidhaminiwa kwa mwaka wa tisa sasa na mdau wa soka wa Rorya, Peter Owino, kupigwa Desemba 5, mwaka huu.



Kikosi cha Wanamaji FC, kinachotarajiwa kuwavaa mabingwa watetezi wa Umoja Cup, Shirati Mji, katika mechi ya nusu fainali ya michuano hiyo, itakayopigwa Uwanja wa Maji Sota, Rorya, Jumapili wiki hii. **NA MPIGACHA WETU**

# Azam FC kicheko Dube kurejea dimbani

**Na Adam Fungamwango**

YUKO fiti! Uongozi wa Azam FC umesema afya ya straika wake tegemeo, Prince Dube imeimarika na sasa yuko 'fiti' kurejea kwenye mikikimikiki ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara ambayo inaelekea kuingia katika raundi ya saba.

Mbali na mechi za Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, Azam FC inajiimarisha ili ifanye vizuri katika mashindano ya Kombe la FA ambayo yatarindima kuanzia mapema mwezi ujao.

Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zacharia 'Zaka Zakazi', alisema jana mshambuliaji huyo ameshaanza mazoezi ya utimamu wa mwili pamoja na wachezaji wenzake na kuna uwezekano mkubwa akaanza kuonekana dimbani hivi karibuni.

Thabit alisema Dube ana nafasi kubwa ya kuonekana kwa mara ya kwanza msimu huu katika mechi ijayo ambapo Novemba 30, mwaka huu, Azam FC itawakaribisha Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi Dar es Salaam.

"Tuko mazoezini, mwalimu ameona mambo hayako sawa kwenye sehemu zote, ulinzi, kiungo na hata ushambuliaji, ndiyo maana utaona timu haifungi sana, lakini imeruhusu mabao sana, ndiyo mambo ambayo mwalimu anayafanyia kazi. Kingine ni kwamba mchezaji wetu Prince Dube kwa sasa amepona. Alikuwa anafanya mazoezi mepesi, kwa sasa anafanya mazoezi magumu ya utimamu wa mwili, hivyo kama atakuwa sawa kwenye mechi ijayo anaweza kucheza," alisema kiongozi huyo.

Nyota huyo wa kimataifa kutoka Zimbabwe alifanyiwa upasuaji wa mguu Septemba mwaka huu katika Hospitali ya Vicent Pellotti jijini Cape Town, Afrika Kusini na Azam ilitangaza angekaa nje ya dimba kwa muda wa wiki sita.

Dube alisajiliwa na Azam Agosti, mwaka jana na amekuwa straika tegemeo kwenye timu hiyo, akimaliza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita akiwa na mabao 14, licha ya kutokuwa dimbani kwa muda mrefu.

Azam itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kuchapwa mabao 2-1 na KMC huku pia ikiwa imetolewa kwenye mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# Polisi, Biashara mechi ya ufundi

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini (pichani chini), amesema mchezo wao unaofuata wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya Biashara United, utakuwa na ushindani kutokana na viwango bora vya wachezaji wa timu zote mbili.

Biashara United itaikaribisha Polisi Tanzania Novemba 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Karume mjini Musoma, mkoani Mara.

Malale aliliambia gazeti hili timu yake imejipanga imara kuelekea katika mechi hiyo na wanatarajia kwenda kuvuna pointi tatu.

Kocha huyo alisema anaifahamu vema Biashara United baada ya 'kuisoma' ilipokuwa inashiriki mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika na sasa iliporejea kwenye mechi za ligi ya nyumbani.

"Utakuwa mchezo mgumu, lakini mzuri, timu zote mbili zinaundwa na wachezaji wanaojua kupambana, wanaocheza kwa kufuata maelekezo zaidi, kucheza na timu ya aina hii ni lazima tuongeze umakini," Malale alisema.



Makamu Mwenyekiti wa timu hiyo, Robert Munisi, aliliambia gazeti hili wamejipanga kwenda mapema Musoma ili kuwapa nafasi wachezaji wao kupumzika na kuwasubiri wenyeji.

"Hatutaki kurudia kilichotokea katika mechi dhidi ya Coastal Union, naamini sisi pia tutashinda ugenini, tutaondoka na pointi, inawezekana, tumeshafahamu tulipojikwaa kwenye mechi iliyopita," Munisi alisema.

Katika msimamo wa ligi, Polisi Tanzania iko nafasi ya tano ikiwa imejikusanyia pointi 10 baada ya kushinda mechi tatu, sare moja na imepoteza michezo miwili.

Yanga yenye pointi 16, ndio vinara wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara wakati mabingwa watetezi ni Simba na wako nyuma yao kwa pointi mbili kwenye msimamo wa ligi hiyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### POCHETTINO KUISUBIRISHA UTD

KLABU ya Manchester United iko tayari kuacha utafutaji wa kocha wa muda wa timu hiyo iwapo wanaweza kumpata Mauricio Pochettino kutoka Paris St-Germain sasa. ***(Guardian)***

### ZIDANE AWEKA MTEGO PSG

KOCHA wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane, ambaye ana uwezekano mkubwa wa kulengwa na Manchester United anataka kuchukua nafasi ya ukocha pale PSG iwapo Mauricio Pochettino ataondoka kuelekea Old Trafford. ***(Telegraph)***

### CAMARA AFUATILIWA LIVER

LIVERPOOL, Leicester na Newcastle United zinamfuatilia kwa karibu mshambuliaji wa Guinea, Aguibou Camara, 20, anayecheza katika klabu ya Olympiakos. ***(Sun)***

### HAALAND NA MKATABA

BORUSSIA Dortmund wanaandaa mkataba mpya kwa ajili ya mshambuliaji, Erling Braut Haaland, 21, katika azma ya kumshawishi mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway kuendelea kubaki katika klabu hiyo. ***(Sky Sport)***

### FERGUSON KUTOHUSIKA UNITED

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Sir Alex Ferguson, ambaye ni mkurugenzi wa bodi ya soka ya klabu hiyo, hatakuwa na jukumu lolote katika kumsaka kocha mpya. ***(ESPN)***

### ZIYECH ATAJWA BARCA

BARCELONA wanataka kumsajili mchezaji wa kimataifa wa Morocco anayeichezea klabu ya Chelsea, Hakim Ziyech, 28, na mshambuliaji Mjerumani Timo Werner mwenye miaka 25, kama wachezaji mbadala kwa mshambuliaji wa Manchester City na England, Raheem Sterling, 26. ***(ESPN)***

### WITSEL ATAKIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United wana nia na kiungo wa kati wa Borussia Dortmund, Axel Witsel, 32, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Sport1)***

### LIVERPOOL KUMZUIA ORIGI

MSHAMBULIAJI raia wa Ubelgiji, Divock Origi, 26, ambaye analengwa na Newcastle, hataruhusiwa kuondoka Liverpool Januari. ***(Northern Echo)***

### KUNG'OLEWA ATLETICO

NEWCASTLE United wanamtaka beki, Kieran Trippier, 31, kutoka Atletico Madrid. ***(Mirror)***

### GERRARD KUMUUZA TRAORE

KOCHA mpya wa Aston Villa, Steven Gerrard, ameidhinisha mauzo ya mchezaji wa kimataifa wa Burkina Faso, Bertrand Traore, 26. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO APAGAWA UNITED WAKIFUZU KWA VILLARREAL

**Sisi ni Man United na kamwe hatutaacha kuipambania klabu! Twendeni, Mashetani!...**

**VILLARREAL,** Hispania

CRISTIANO Ronaldo amesisitiza Manchester United "kamwe haitaacha kupambana" baada ya nyota huyo kuiwezesha klabu hiyo kufuzu hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku akivunja rekodi.

Ronaldo amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga mfululizo kwenye mechi tano za kwanza za Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa timu ya England, wakati United ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Villarreal katika mchezo wa Kundi F, juzi Jumanne.

Ikicheza mechi yake ya kwanza bila ya kocha, Ole Gunnar Solskjaer, ambaye ametimuliwa na sasa kikosi kipo chini ya Michael Carrick, Ronaldo alifunga bao la uongozi dakika ya 12 likiwa bao la 799 kwenye maisha yake ya soka kabla ya mchezaji mwenzake, Jadon Sancho kufunga la pili.

**Kulikuwa na changamoto ndani ya kikosi cha United, ambacho kilishinda mechi mbili tu kati ya nane zilizopita wakati kikielekea mchezo huo, na Ronaldo ameelezea morali ya timu hiyo.**

"Mara zote najisikia vizuri nikicheza nchini Hispania, inavutia kushinda Hispania, nimeridhika kufunga Hispania, nchi ambayo mara zote huwa najisikia mtu wa aina yake," alisema Ronaldo akiandika kupitia kwenye mitandao yake ya kijamii.

"Hongera kwa wachezaji wote, tumepambana na ushindi umetuweka pale tunapostahili kuwapo!

"Sisi ni Man United na kamwe hatutaacha kuipambania klabu! Twendeni, Mashetani!"

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 amefunga mabao sita kwa United msimu huu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya; akizidiwa na Ruud van Nistelrooy tu aliyefunga mabao nane msimu wa 2004-05.


MECHI KALI
HOME
AWAY
BAYER LEVERKUSEN
1.48 | 4.68 | 5.78
CELTIC

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 710

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
halopesa
airtel money
EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DE JONG ATAJWA KUMRITHI POGBA



**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Manchester United imeripotiwa kuwa inafikiria kumsajili nyota wa Barcelona, Frenkie de Jong kama mbadala wa Paul Pogba.

'Mashetani Wekundu' hao hadi sasa hawajafikia muafaka wa makubaliano ya mkataba mpya na nyota wao, Pogba.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, anafikia mwisho wa mkataba wake wa sasa msimu ujao wa majira ya joto.

Man United wapo mbioni kumpoteza nyota huyo kama mchezaji huru msimu ujao wa majira ya joto, wakati De Jong akihusishwa na kuondoka Barcelona katika siku za hivi karibuni huku akitajwa kuwa na thamani ya euro milioni 75.

Klabu nyingi za Ligi Kuu England zinamtupia macho nyota huyo wa kimataifa wa Uholanzi na huenda kukawa na mshike mshike kwenye dirisha la uhamisho la Januari.

Kwa mujibu wa Daily Mail, Man United wanajiandaa kupambana na Manchester City na Liverpool kuiwania saini ya De Jong ambaye anaweza kuwa sokoni Januari.



# *Thiago hana mpango kurudi Barcelona*

**LIVERPOOL,** England

KIUNGO wa Liverpool, Thiago Alcantara, hajafikiria kurudi Barcelona, akisisitiza kuwa "kwa asilimia 100 nina furaha" kuchagua kucheza pale Anfield.

Thiago amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara tangu alipohamia Liverpool akitokea Bayern Munich mwaka 2020.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania, alikabiliwa na majeraha ya kifundo cha mguu baada ya kuumizwa na Richarlison wa Everton katika mchezo wake wa kwanza kuanzia Oktoba mwaka jana.

Alicheza mechi 24 za Ligi Kuu msimu uliopita, akianza 20 kati ya hizo na amefunga mara moja.

Majeraha zaidi yamemwandama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, akicheza mechi nane tu kwenye mashindano yote msimu huu.

Baada ya Xavi kuchukua mikoba ya Ronald Koeman pale Barca, kumekuwa na uvumi unaomhusisha Thiago kurudi klabuni hapo.

## HABARI MICHEZO


# ,494,580

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 27/11/21 | 18:00 | Crystal Palace vs Aston Villa | 2.18 | 3.30 | 3.35 |
| 02. 27/11/21 | 18:00 | Hull City vs Millwall | 2.70 | 3.09 | 2.60 |
| 03. 27/11/21 | 18:00 | Huddersfield vs Middlesbrough | 2.46 | 3.10 | 2.85 |
| 04. 27/11/21 | 20:00 | Juventus vs Atalanta | 2.22 | 3.46 | 3.12 |
| 05. 27/11/21 | 20:30 | Mallorca vs Getafe | 2.43 | 2.90 | 3.30 |
| 06. 27/11/21 | 20:30 | Cercle Brugge vs Mechelen | 2.66 | 3.45 | 2.44 |
| 07. 27/11/21 | 20:45 | Fortuna Sittard vs Groningen | 2.72 | 3.26 | 2.47 |
| 08. 27/11/21 | 23:00 | Villarreal vs Barcelona | 2.69 | 3.33 | 2.57 |
| 09. 28/11/21 | 15:30 | Nurnberg vs St. Pauli | 2.60 | 3.23 | 2.60 |
| 10. 28/11/21 | 17:00 | Brentford vs Everton | 2.38 | 3.20 | 3.05 |
| 11. 28/11/21 | 17:00 | Bordeaux vs Brest | 2.42 | 3.34 | 2.84 |
| 12. 28/11/21 | 18:15 | Espanyol vs Real Sociedad | 3.30 | 3.25 | 2.22 |
| 13. 28/11/21 | 18:30 | Maritimo vs Pacos Ferreira | 2.66 | 3.10 | 2.66 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 25 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 1796 | KF Gjilani vs KF Drita | 2.24 | 3.08 | 3.03 |
| 15:00 | 3135 | KF Ballkani vs Malisheva | 1.58 | 3.48 | 5.61 |
| 15:00 | 3665 | KF Drenica Skenderaj vs KF Llapi | 2.67 | 2.91 | 2.62 |
| 15:45 | 3328 | Deportivo Maldonado vs CS Cerrito | 2.42 | 3.38 | 2.56 |
| 16:00 | 1803 | El Ittihad Alexandria vs Farco FC | 2.09 | 3.16 | 3.56 |
| 16:30 | 3487 | NA Hussein Dey vs MC Oran | 1.68 | 3.28 | 5.02 |
| 16:30 | 4293 | Mladost Lucani vs Vojvodina | 3.32 | 3.51 | 1.94 |
| 16:30 | 5564 | CS Constantine vs MC Alger | 1.92 | 3.07 | 3.94 |
| 17:00 | 4338 | Northeast United FC vs Kerala Blasters FC | 2.04 | 3.32 | 3.23 |
| 17:30 | 5805 | Al Fateh (KSA) vs Dhamk | 2.68 | 3.42 | 2.48 |
| 18:00 | 4825 | Rapide Oued Zem vs Mouloudia Oujda | 2.95 | 3.10 | 2.49 |
| 18:30 | 1010 | Flora Tallinn vs Partizan | 5.81 | 4.41 | 1.51 |
| 18:30 | 3031 | Ceramica Cleopatra vs Zamalek | 5.12 | 3.00 | 1.83 |
| 18:30 | 4834 | Kairat Almaty vs FC Basel | 4.00 | 3.65 | 1.87 |
| 19:00 | 4146 | ES Setif vs CR Belouizdad | 2.01 | 3.17 | 3.50 |
| 19:40 | 2520 | Al Shabab Riyadh vs Al Raed Club | 1.72 | 3.76 | 4.46 |
| 20:15 | 3348 | Hassania Agadir vs Olympique Khouribga | 2.15 | 3.03 | 3.27 |
| 20:45 | 1725 | Bayer Leverkusen vs Celtic | 1.48 | 4.68 | 5.78 |
| 20:45 | 2498 | NK Mura vs Tottenham | 15.06 | 7.03 | 1.17 |
| 20:45 | 2578 | Lokomotiv Moscow vs Lazio | 4.20 | 3.60 | 1.84 |
| 20:45 | 2784 | HJK Helsinki vs Alashkert Martuni | 1.46 | 4.49 | 6.59 |
| 20:45 | 2873 | Betis vs Ferencvaros TC | 1.22 | 6.44 | 12.07 |
| 20:45 | 2966 | Rennes vs Vitesse Arnhem | 1.44 | 4.60 | 6.79 |
| 20:45 | 3124 | Karabakh vs Omonia Nicosia | 1.64 | 3.86 | 5.21 |
| 20:45 | 3195 | Galatasaray vs Marseille | 2.79 | 3.34 | 2.49 |
| 20:45 | 3608 | Maccabi Haifa vs Union Berlin | 2.90 | 3.55 | 2.30 |
| 20:45 | 4131 | Slovan Bratislava vs PAOK | 2.81 | 3.63 | 2.33 |
| 20:45 | 4216 | Dinamo Zagreb vs Racing Genk | 2.39 | 3.45 | 2.85 |
| 20:45 | 4419 | Slavia Prague vs Feyenoord | 2.27 | 3.50 | 3.00 |
| 20:45 | 4936 | Rapid Vienna vs West Ham | 5.01 | 4.10 | 1.62 |
| 20:45 | 5310 | Midtjylland vs Sporting Braga | 2.50 | 3.36 | 2.76 |
| 20:45 | 5608 | Lincoln FC vs Copenhagen | 12.43 | 5.95 | 1.23 |
| 20:45 | 5933 | Red Star Belgrade vs Ludogorets Razgrad | 1.36 | 4.91 | 8.21 |
| 21:00 | 3882 | Al Ahly Cairo vs Smouha Club | 1.35 | 4.92 | 7.68 |
| 22:00 | 4440 | Republic of Ireland W vs Slovakia W | 1.57 | 4.10 | 5.60 |
| 22:30 | 2041 | CA Progreso vs CA Penarol | 4.72 | 3.66 | 1.63 |
| 23:00 | 1455 | Leicester vs Legia Warszawa | 1.17 | 7.20 | 15.00 |
| 23:00 | 2303 | Randers vs CFR Cluj | 2.12 | 3.50 | 3.30 |
| 23:00 | 2766 | Roma vs Zorya Lugansk | 1.18 | 7.19 | 13.97 |
| 23:00 | 3388 | Maccabi Tel Aviv vs LASK Linz | 2.27 | 3.71 | 2.86 |
| 23:00 | 3541 | Arsenal Sarandi vs Union Santa Fe | 3.03 | 3.03 | 2.27 |
| 23:00 | 3795 | Anorthosis Famagusta vs KAA Gent | 4.70 | 3.90 | 1.69 |
| 23:00 | 3829 | Monaco vs Real Sociedad | 2.50 | 3.36 | 2.76 |
| 23:00 | 4006 | Olympiakos vs Fenerbahce | 1.82 | 3.69 | 4.19 |
| 23:00 | 5110 | PSV Eindhoven vs Sturm Graz | 1.20 | 6.61 | 13.02 |
| 23:00 | 5134 | Bodo Glimt vs CSKA Sofia | 1.23 | 6.02 | 12.03 |
| 23:00 | 5295 | Brondby vs Lyon | 3.24 | 3.54 | 2.13 |
| 23:00 | 5438 | Baumit Jablonec vs AZ Alkmaar | 3.80 | 3.95 | 1.84 |
| 23:00 | 5716 | Rangers vs Sparta Prague | 1.81 | 3.65 | 4.30 |
| 23:00 | 5937 | Eintracht Frankfurt vs Royal Antwerp | 1.39 | 5.01 | 7.02 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# POCHETTINO AZUNGUMZIA TETESI KUTUA MAN UNITED

**PARIS,** Ufaransa

MAURICIO Pochettino amesema majaliwa yake "hayana shaka" kwani ana furaha pale Paris Saint-Germain huku ripoti zikimhusisha na Manchester United kwenda kuchukua nafasi ya Ole Gunnar Solskjaer.

United walimfukuza Solskjaer Jumapili baada ya kufungwa mabao 4-1 na Watford kwenye mchezo wa Ligi Kuu England na Michael Carrick amechukua nafasi ya kuisimamia timu hiyo kwa muda.

'Mashetani Wekundu' hao waliripotiwa kupanga kuteua kocha wa muda hadi mwishoni mwa msimu huu, lakini uvumi umeongezeka kwamba wanafanya mazungumzo na Pochettino ili kupewa mikoba hiyo.

Kocha wa zamani wa Tottenham Hotspur, Pochettino alisisitiza haangalii uwezekano wa kuondoka PSG.

Aliwaambia waandishi wa habari Jumanne: "Nafikiri ilikuwa wazi kabisa. Nilisema kwamba, nina mkataba hadi mwaka 2023. Msimu huu na msimu unaokuja.




Mshindi wa Bonasi ya Sportpesa, Aichat Haroun Abdallah (23) kutoka Kigamboni, DSM akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 6.7 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 11 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. Jackpot ya wiki hii inayoshindaniwa imefika shilingi 710,494,580. **PICHA: SPORTPESA**

# *Xavi: Lazima tukaichape Bayern*

**BARCELONA,** Hispania

XAVI amesema kwamba, Barcelona lazima ikashinde mchezo wake dhidi ya Bayern Munich kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, baaada ya juzi, Jumanne kutoka sare ya bila kufunga na Benfica.

'Blaugrana' hao walikosa nafasi ya kufuzu hatua ya mtoano kwenye michuano hiyo, licha ya kutawala mchezo pale kwenye dimba la Camp Nou. Ingawa Xavi alikuwa kocha wa 13 mfululizo kuepuka kipigo kwenye mchezo wake wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kuiongoza Barca, lakini kikosi chake kilishindwa kuwafunga Benfica.

Matokeo hayo yakawafanya kuwa nafasi ya pili kwenye msimamo wa Kundi E wakiwazidi pointi mbili Benfica waliopo nafasi ya tatu, lakini wanakabiliwa mchezo wa mwisho dhidi ya Bayern Munich wiki mbili zijazo ambao utaamua hatima yao.

Xavi alisisitiza kikosi chake kitasafiri kwenda Ujerumani kikiwa na lengo moja tu la kuhakikisha kinapata ushindi na si vinginevyo.

# Michezo

Alhamisi Novemba 25, 2021

Nipashe





Ronaldo apagawa Utd wakifuzu

UKURASA 21


# Aucho aituliza Yanga, Chama atoa msimamo

●●● Sasa ataka kuvunja mkataba wake Morocco ili kutua tena nchini kukipiga...

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI kiungo Mzambia, Clatous Chama akifunguka hayuko tayari kujiunga na Yanga, mchezaji nyota wa kimataifa kutoka Uganda, Khalid Aucho ameweka wazi hana mpango wa kuondoka kwa vinara hao wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara.

**Aucho ameliambia gazeti hili yeye bado ni mchezaji wa Yanga na tetesi zinazosambaa kuwa anajiandaa kuachana na waajiri wake hao, si za kweli.**

"Sina mpango wa kwenda kokote, mimi bado ni mchezaji wa Yanga," Aucho alisema kwa kifupi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema klabu yao iko tayari kufanya mazungumzo na timu yoyote ndani au nje ya Tanzania ambayo inahitaji huduma ya Aucho. Bumbuli alisema Yanga bado ina mkataba na Aucho, lakini inakaribisha ofa kutoka kwa timu yoyote na inawakumbusha viongozi wa klabu nyingine kufuata taratibu na si kutumia njia za 'panya'.

"Tunasikia maneno maneno tu huko, lakini niwaambie tu Aucho ana mkataba wa miaka miwili na Yanga, tunafahamu huyu ni mchezaji mzuri na zipo timu zinamtolea macho, tunawaambia tu walete ofa yao tuone tunafanyaje, huyu ni mchezaji wa Yanga," alisema Bumbuli.

Kiongozi huyo alisema wanachana na mashabiki wa Yanga wasiwe na hofu yoyote juu ya kumpoteza mchezaji huyo kwa sababu bado ni mali yao kwa mujibu wa mkataba ambao alisaini na klabu hiyo.

"Unajua kila tunapoelekea kwenye dirisha la usajili, maneno mengi yanatokea, mashabiki wetu wasishtushwe na kelele hizi, wachezaji wote wana mikataba na hakuna mchezaji atakayeondoka kiholela," alisema Bumbuli.

Wakati hali kwa Aucho ikiwa hivyo, Chama amelazimika kuweka wazi mustakabali wake baada ya kuwapo mgongano wa mawazo kati yake na wakala wake ambaye anahitaji kuona anajiunga na Yanga endapo ataondoka kwa mkopo RS Berkane ya Morocco.

Taarifa zinaeleza baada ya Chama kuwa na wakati mgumu huko Morocco, anajipanga kuvunja mkataba na Waarabu hao na chaguo lake la kwanza ni kurejea Simba licha ya ofa nono inayotaka kutolewa na Yanga.

Mapema wiki hii kumekuwa na tetesi mbalimbali za usajili huku Chama akihusishwa na kutua Yanga na Aucho akitajwa kuwa mbioni kuondoka katika klabu hiyo katika kipindi cha dirisha dogo la usajili kinachotarajiwa kufunguliwa Desemba 15, mwaka huu.

Na Yanga imetoa kauli hiyo ikiwa ni siku mbili tu zimepita baada ya kuanguka katika kesi ya kimkataba waliyofungua katika Mahakama ya Usuluhishi ya Masuala ya Michezo (CAS), dhidi ya mchezaji wao wa zamani, Mghana Bernard Morrison ambaye kwa sasa anaichezea Simba.



AUCHO

# Pablo aisoma Red Arrows, afunguka

**Faustine Feliciane na Saada Akida**

ZIKIWA zimebakia siku tatu kabla ya kukutana na Red Arrows ya Zambia kwenye mechi ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, amesema anahitaji kuongeza umakini kwenye kikosi chake ili kuhakikisha wanasonga mbele katika michuano hiyo.

Simba, wawakilishi pekee wa Tanzania waliobaki katika mashindano ya kimataifa, wanatarajia kuikaribisha Red Arrows Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili, Pablo alisema baada ya kuona ubora na udhaifu wa wapinzani wao, Reds Arrows, amejipanga kukiimarisha zaidi kikosi chake ili kupata matokeo mazuri katika mchezo huo wa kwanza na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kumaliza kazi watakapokwenda ugenini.

Pablo alisema anawaamini wachezaji wake wanauwezo wa kupambana na kumpa matokeo chanya katika mechi hiyo ya kimataifa pamoja na Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara ambayo inaendelea.

Alisema kwa muda ambao amekaa na wachezaji wake, amebaini wana mwelekeo mzuri na wameshaanza kucheza kwa kufuata falsafa yake ya umiliki wa mpira na kucheza soka la 'pasi nyingi'.

"Tumepata nafasi ya kuwaangalia wapinzani wetu na kujua ubora na mapungufu yao, vyote tunavifanyia kazi, tunajua mchezo utakuwa wa ushindani mkubwa kwa kila mmoja wetu, tunapambana kusaka ushindi, kwa upande wetu tunahitaji kushinda nyumbani," alisema Pablo.

Aliongeza mechi hiyo itakuwa ngumu na wanapaswa kucheza kwa kujitolea asilimia 100 katika muda wote wa dakika 90 ili kufikia malengo na si vinginevyo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >